epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumatano Juni 26, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581719
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

UKURASA WA 2

**Baadhi** wagoma Kariakoo, wengi wafungua maduka; Mwanza wafunga



UKURASA WA 3

**Sita** wapitishwa mchuano urais TLS, Mwabukusi, Kapteni Bendera...

UKURASA WA 19

**Hali** bado tete maandamano Kenya, maduka na barabara zake zafungwa



UKURASA 21

**MODRIC: BADO NATAKA KUENDELEA KUCHEZA TU**

# Mbowe: Umasikini wetu unaanzia hapa

• **Achambua** kinachotoka na kinachoingia nchini... *Endelea ukurasa 2*



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, akizungumza na wananchi katika mkutano wa hadhara uliofanyika mjini Mbulu, mkoani Manyara, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## ‘Wafoji’ namba kuwahi foleni kliniki ya Makonda

UKURASA 5

## Watatu wa familia moja wafa ajalini wakitoka kwenye harusi

• **Wamo** mama, shangazi wa bwana harusi... *Ukurasa 5*

**MICHEZO** **YANGA SC KUSHUSHA BEKI LA ENYIMBA** UK.24 **KATUNI** UK.6



Mhariri Mtendaji wa Gazeti la The Guardian, Wallace Mauggo (wa pili kulia), akifafanua jambo kuhusu utendaji kazi katika chumba cha habari kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa kampuni ya Helium One Global Ltd, Lorna Blaisse (wa tatu kulia), na Mkurugenzi wa Fedha na Biashara wa kampuni hiyo, Graham Jacobs (kushoto), walipotembelea ofisi za The Guardian Ltd (TGL) wachapishaji wa magazeti ya The Guardian na Nipashe, Mikocheni Dar es Salaam jana. Wengine ni Mkurugenzi wa Biashara wa TGL, Ajay Goyal (kulia) na Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe. **PICHA: JOHN BADI**

# Mbowe: Umaskini wetu unaanzia hapa

**Na Godfrey Mushi,** BABATI

MWENYEKITI wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, ameibua hoja ya kupaa gharama za maisha nchini, akichambua hali ya maisha Tanzania na nchi jirani ya Kenya.

Alisema hali hiyo inasababisha maumivu kila mahali, kutokana na bidhaa muhimu kupanda bei.

Akizungumza jana na wananchi wa Minjingu katika Wilaya ya Babati mkoani Manyara, Mbowe alitaja mambo yanayochochea kupaa kwa gharama za maisha nchini kuwa ni pamoja na malori yanayotoka nchi jirani, kuachwa yakizunguka mashambani yakichukua malighafi za viwandani na kusafirishwa kwenda nje ya nchi.

"Angalia malori yanayokwenda Kenya, yamebeba bidhaa za mashambani. Yamebeba nyanya za Tanzania, yamebeba vitunguu vya Tanzania, yamebeba mahindi ya Tanzania, yamebeba maharage ya Tanzania, yamebeba parachichi, yamebeba kabeji, yamebeba mboga, kila kitu wanapeleka Kenya.

"Ukiangalia malori yanayotoka Kenya kuja Tanzania, yamebeba bidhaa za viwandani. Maana yake ni nini, kwamba Tanzania tunauza mahindi kwa mfano shilingi 1,000 tunawauzia Wakenya.

...Wananunua mahindi wanakwenda kuyatengeneza wanasaga, unakuwa unga wa mahindi, ama unga wa lishe wanaturudishia Watanzania. Mahindi kilo waliyonunua Sh. 1,000 Tanzania yakienda Kenya viwanda vya Kenya, vya vijana wa Kenya vinafanya kazi, Wakenya wanapata kazi. Halafu wanarejesha mahindi Namanga, yakiwa ni unga wanatuuzia Watanzania kilo moja zaidi ya Sh. 3,000."

Aidha, alisema machungwa kutoka Tanga, tani kwa tani, malori ya mizigo aina ya Fusso kuanzia 20 mpaka 30 yanaenda Kenya, yanachukua matunda wanakwenda kuyachakata, wanakamua juisi (sharubati) wanaweka kwenye chupa na kwenye vipaketi, wanatia kwenye malori na wanawarudishia Watanzania.

"Yaani aliyetuloga sijui ni nani! Kwa hiyo matunda yakienda Kenya, wanapata ajira vijana wao. Tunatamani vijana wa Tarangire, Minjingu wenye jeuri ya kusimama na kutetea nchi yao na kutetea malaika wa Mungu wao.

Aidha, Mbowe alidai kuwa bidhaa kutoka upande wa Kenya, zina unafuu kwa asilimia 40 ikilinganishwa na Tanzania, kwa kuwa mfuko wa saruji wa kilo 50, Kenya wananunua kwa Sh. 9,000 na wakija Tanzania, wananunua kwa Sh. 22,000.

Vilevile, Mbowe alidai kuwa sukari ya Kenya ni Sh. 1,600 ya Tanzania, na wakiileta Tanzania ni Sh. 5,000 na ukikutwa nayo ni jela.

### UMASIKINI

Kuhusu hali ya umasikini katika eneo la Minjingu, Mbowe alisema: "Huu Mji wa Minjingu ulijengwa na kiwanda hiki, nyumba nzuri mnazoziona Minjingu zilijengwa na kiwanda hiki. Jana (juzi) nilikuwa pale Namanga (Wilaya ya Longido), ukienda pale kuna jambo linaumiza sana.

"Ni hivi ndugu zangu, Kenya na Tanzania ni ndugu na ni majirani, Wamasai wa Kenya, ndio Wamasai wa Tanzania. Ardhi yetu na ardhi yao ni sawasawa.

Ukienda Namanga unaiona Kenya hiyo na Kenya wanaiona Tanzania hii. Nilifika Namanga jana, ninawauliza wananchi, mna maisha gani hapa mkilinganisha na Kenya?

...Wakaniambia 'Mwenyekiti, wala huwezi kulinganisha'. Nikawauliza 'kwanini? Wakaniambia 'upande wa Kenya, wana maji kwenye kila kaya, kila nyumba ina maji ya bomba ni safi na salama.

Upande wa Tanzania hatuna maji'. Jana waliniambia upande wa Kenya wana umeme saa 24, wakaniambia 'hapa upande wa Tanzania tunaweza kwenda hadi wiki mbili tatu hatujaona umeme'.

...Wakaniambia 'watoto wetu wote wale wenye uwezo wanavuka mpaka kwenda kwenye shule za Kenya, lakini hakuna mtoto hata mmoja anayetoka kuja kusoma Tanzania," Mbowe alisema katika mkutano huo.

### WAZIRI MKUMBO

Juni 13 mwaka huu, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, akiwasilisha bungeni Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2024/25, alitaja mambo matano yanayoonesha kuwapo tatizo kiuchumi nchini.

Alitaja mambo hayo matano ni pamoja na: Ukuaji uchumi umekuwa ukihusisha sekta chache na ambazo haziajiri watu wengi kutoka kaya maskini; na ukuaji uchumi nchini umekuwa unategemea uwekezaji wa umma katika miundombinu huku sekta binafsi haijaonekana kuchukua nafasi yake kikamilifu katika kuchochea ukuaji uchumi kama ilivyotarajiwa.

Waziri huyo alitaja jambo lingine ni Tanzania inanunua zaidi kutoka nje kuliko kiwango inachouza. Hivyo, bado kuna urari mkubwa katika biashara.

"Kwa mfano, thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi kwa mwaka 2023 ilikuwa Dola za Marekani bilioni 8.2 kulinganisha na thamani ya ununuzi wa bidhaa ambazo Tanzania iliagiza kutoka nje ya nchi ya Dola bilioni 13.7.

"Hii ndiyo kusema nchi yetu bado inatumia fedha nyingi za kigeni kuagiza bidhaa ambazo zingeweza kuzalishwa nchini," alisema Waziri Mkumbo na kufafanua kuwa uchumi umekuwa ukikua kwa kasi zaidi katika maeneo ya mijini kuliko vijijini.

# Kariakoo baadhi wagoma, wapo waliofungua; Mwanza wafunga

**Na Waandishi Wetu**

WAFANYABIASHARA wa Soko la Kimataifa la Kariakoo jijini Dar es Salaam jana wamefungua maduka na kuendelea na biashara baada ya serikali kusitisha ukaguzi wa risiti za kielektroniki na ritani za kodi iliyokuwa ikifanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Asilimia ndogo ya wafanyabiashara hao, waliendelea kufunga maduka yao wakiitaka serikali kutekeleza kwa vitendo ilichoahidi.

Wakizungumza na mwandishi wa habari hii sokoni hapo, baadhi ya wafanyabiashara waliofungua maduka yao walisema wamefanya hivyo kwa kuamini kwamba, serikali itatekeleza kwa vitendo iliyoahidi katika kikao kilichofanyika baina yake na viongozi wa wafanyabiashara.

"Jana (juzi) serikali iliahidi mwezi ujao itatatua matatizo yetu, tunaomba ifanye hivyo kwa vitendo, wapo wenzetu ambao bado hawajafungua, lakini sisi wengine tunaamini serikali tunaomba isituangushe itekeleze," alisema Ruben Kaiza, mfanyabiashara wa duka la jumla la vipodozi.

Lucas Amon, mfanyabiashara wa nguo, alisema kero nyingine kubwa TRA kufilisi akaunti za wafanyabiashara.

"Tunaomba hizi sheria kandamizi zinazoipa TRA kufanya hivi hazifai ziondolewe, zinatuumiza sana wafanyabiashara wengi," alisema Amon.

Baadhi ya wafanyabiashara ambao walikutwa wakiwa wameketi nje ya maduka yao yakiwa yamefungwa, walisema wanachosubiri ni utekelezaji wa ahadi iliyotolewa na serikali.

Baadhi ya wateja waliokutwa sokoni hapo akiwamo, Halima Ashraf, walishukuru hatua ambazo serikali imechukua na kuhakikisha huduma kurejea.

"Tunashukuru leo (jana) tumepata bidhaa kwa maana jana (juzi) tulikuja tukakosa. Bidhaa nyingi tulizohitaji tumepata isipokuwa madera ndio tumekosa kwa sababu tumekuta maduka yamefungwa," alisema Halima.

Katibu wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Mkoa wa Dar es Salaam, Riziki Ngaga, alisema tamko la viongozi linawaomba wafanyabiashara kufungua maduka yao kwa kuwa serikali imeahidi kutekeleza ilichowaahidi.

### MWANZA

Wakati wafanyabiashara wa Dar es Salaam wakimaliza matatizo yao na serikali, mkoani Mwanza wamefunga maduka yao wakidai hadi kilio chao cha utitiri wa kodi kifanyiwe kazi.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara wa Mkoa wa Mwanza, Patrick Masagati, alisema hawatafanya biashara yoyote mpaka kodi isiyo rafiki kwa biashara zao zitakapoondolewa.

"Tumechoka kusikia matamko ya serikali, tunahitaji mabadiliko ya sheria, yatakayokuwa na tija kwa pande zote mbili na si vinginevyo," alisema Masagati.

Alisema viongozi wamefanya sehemu yao, lakini wafanyabiashara wameamua kugoma, ili kuishinikiza serikali ichukue hatua za kumaliza tatizo hilo.

"Jana na juzi, kulikuwa na vikao huko Dodoma, baina ya viongozi wa wafanyabiashara na uongozi wa serikali, majibu yaliyotolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, ndiyo yaliyopelekea mgomo huu," alisema Masagati.

***Imeandaliwa na Rose Jacob (MWANZA) na Elizabeth Zaya (DAR)**

HABARI KITAIFA

## TAMWA yamlilia Pudenciana Temba

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), Joyce Shebe, amesema amepokea kwa masikitiko taarifa za kifo cha aliyekuwa mhariri wa gazeti la Daily News, Pudenciana Temba, ambaye ni miongoni mwa wanahabari wanawake aliyetumikia tasnia ya habari kwa weledi mkubwa.

Pudenciana alifariki dunia jana katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) alikokuwa akipatiwa matibabu kwa muda mrefu. Akimwelezea alivyomfahamu, Joyce alisema alijipambanua hadi kufikia ngazi ya uhariri, akifanya kazi katika tasnia hiyo takribani miaka 30, akiandikia gazeti la Daily News.

"Mpaka anafariki alikuwa amefikia ngazi ya uhariri kwenye magazeti ya serikali TSN. Kwa upande wa TAMWA amekitumikia kwa uadilifu akiwa ni kundi la pili katika wale waliojiunga TAMWA, ukiachilia mbali waanzilishi," alisema.

Joyce alisema ameshiriki katika harakati nyingi za TAMWA ikiwamo miradi mbalimbali, mafunzo na alijipambanua katika eneo la sekta ya afya.

Joyce alisema pengo lake ni kubwa kwa kuwa katika eneo la habari za Kiingereza, wanahabari wengi hawakimbilii huko, hivyo walitamani aendelee kuwapo ili kuwanoa zaidi.

# 6 wapitishwa urais TLS, wamo Mwabukusi, Kapteni Bendera

**Na Restuta James**

MAWAKILI sita, akiwamo mwanaharakati wa haki za binadamu, Boniface Mwabukusi, wameteuliwa kuwania kiti cha urais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS).

Taarifa ya TLS kwa umma inataja mawakili sita walioteuliwa kuwania urais, orodha hiyo ikiwa na jina la Mwabukusi, akichuana na Wakili Kapteni Ibrahim Bendera, aliyebobea katika sheria zinazohusu bahari.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo iliyotolewa juzi, Juni 24, walioteuliwa kuwania urais mbali na Mwabukusi anayetoka mkoani Mbeya na Kapteni Bendera anayetoka Ilala, ni Emmanuel Muga (Ilala), Revocatus Kuuli (Mzizima), Paul Kaunda (Kanda ya Magharibi), Sweetbert Nkuba (Kinondoni).

**MWABUKUSI**

Ni mwanaharakati wa haki za binadamu, utawala bora na haki ardhi. Ndiye aliyefungua kesi dhidi ya serikali kupinga makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na kampuni ya DP World kuendesha Bandari ya Dar es Salaam.

**KAPTENI BENDERA**

Huyu ni wakili mbobevu katika sheria zinazohusu bahari. Anakumbukwa zaidi katika kesi ya watuhumiwa wa meli ya uvuvi ya Tawariq 1, maarufu Samaki wa Magufuli, iliyokamatwa nchini Machi 2009.

Katika kesi hiyo, Kapteni Bendera alishinda serikali na wateja wake kudai fidia ya meli iliyokuwa na thamani ya Dola za Marekani 2,300,000 (uthamini wa mwaka 2008) pamoja na Sh. 2,074,249,000 ambazo ni gharama za tani 296.3 za samaki.

Ana Shahada ya Uzamili katika Sheria kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, akisomea Sheria za Bahari na Kazi. Pia ana Shahada ya Kwanza ya Sheria) kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

**REVOCATUS KUULI**

Huyu amebobea katika sheria za kiraia na jinai, za kimataifa, haki za binadamu, upatanishi, usuluhishi na masuala ya katiba.

**NKUBA**

Wakili Sweetbert Nkuba amebobea katika kesi za madai, akitumia maendeleo ya kiteknolojia kuwafikishia wananchi huduma za kisheria. Ndiye mwanzilishi wa WakiliApp ambayo ni akili bandia ya kutoa msaada wa kisheria.

**PAUL KAUNDA**

Wakili huyu ni mbobevu wa sheria za bima, biashara na ufilisi.

Mbali na kiti cha urais, taarifa ya TLS ina jina la Laetitia Ntagazwa (Iringa), aliyeteuliwa kuwania nafasi ya makamu wa rais.

Inaelezwa katika taarifa hiyo kuwa Aziza Msahi (Ilala), hakustahili kuchaguliwa kwa mujibu wa kifungu cha 15 (3)(d) cha Sheria ya Chama cha Wanasheria Tanganyika, Sura 307, kama ilivyorekebishwa na Sheria ya Sekta (Marekebisho Mengineyo) Na. 11 ya 2023.

Vifungu hivyo vinambana wakili huyo kwa kuwa haendeshi au kusimamia kampuni ya mawakili yenye wafanyakazi watano au zaidi wanaohudumu katika bodi yoyote ya uongozi inayotambuliwa.

Katika nafasi ya mweka hazina, aliyeteuliwa ni Stella Rweikiza (Kinondoni), wakati wa nafasi ya Mwenyekiti Chama cha Wanasheria Vijana (AYL) walioteuliwa ni Emmanuel Ukashu (Ilala), Denis Eliasaph (Kinondoni), huku Victor Kweka (Dodoma), Joseph Lameck na Moses Misiwa (Mwanza) wakikosa sifa kwa mujibu wa kanuni mbalimbali za chama hicho.

Kutangazwa majina hayo kunatoa nafasi ya wateuliwa kuanza kampeni Jumamosi ya Julai 6 hadi Agosti Mosi mwaka huu na uchaguzi unatarajiwa kufanyika Agosti 2, mwaka huu jijini Dodoma.


Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# Elimu kuhusu VVU/Ukimwi kwa wasichana ipewe kipaumbele

**Halfani Chusi na Maria Seme**

TAKWIMU za Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS) zinaonesha wasichana wenye umri wa kuanzia miaka 15 hadi 24 ndiyo kundi hatarishi zaidi kwa maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU).

Kulinda kundi hilo, Ofisa Miradi wa Shirika la Msichana Initiatives, Rosemary Richard (pichani) ameshauri serikali na wadau kuongeza wigo wa kuelimisha jamii hususani kwa wasichana wadogo ili wajilinde dhidi ya maambukizi ya virusi hivyo.

Mkoani Dar es Salaam juzi, Rosemary alitoa rai hiyo alipowakutanisha wanaharakati na wasichana viongozi kutoka mikoa minne kutafakari maendeleo ya harakati za kifeminia Afrika na duniani kwa ujumla.

Rosemary alisema kupitia mradi wao wa 'Sauti Yetu Nguvu Yetu', unaokutanisha wasichana mbalimbali kwa lengo la kuweka mikakati ya pamoja katika kupambana na ukatili wa kijinsia na kupeana elimu ya kujikinga na VVU, wamebaini wengi hawana elimu ya kutosha kujikinga na maradhi hayo.

Alisema mradi huo unatekelezwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Dodoma (Kongwa) na Tabora, ukilenga kupata wafadhili watakaowezesha kuifikia mikoa mingine kutengeneza wasichana watakaobeba ajenda ya kuzuia ukatili wa kijinsia, kutetea usawa na kupinga mifumo dume.

"Siku chache zilizopita tulisikia wasichana wadogo ndio wanaongoza kwa maambukizi ya VVU. Katika kupambana na hili, pia tumeamua kuwapa elimu wasichana viongozi watakaoweza kuelimisha na wengine katika kujilinda na madhila hayo," alisema.

Alisema imani potofu kwa baadhi wanaowafikia - kuamini wanataka kubadilisha mila na desturi zao, ni miongoni mwa vikwazo vinavyowakabili katika kutekeleza mradi huo.

"Tunapowafikia mtaani, wengine tunaonekana kama tunapotosha jamii na wengine wanaamini tunaharibu mila na desturi zao, wakati lengo letu ni kupambania haki na usawa katika jamii," alisema



Msichana Kiongozi ambaye ni mnufaika wa mradi huo kutoka Bagamoyo, mkoani Pwani, Mariam Rajabu, alisema elimu aliyopata kupitia mradi huo imemwezesha kusimamia na kuwatetea wasichana wengine kuhusiana na mila potofu na ukatili wa kijinsia.

Alisema kuwa wakati anaingia katika mradi huo, alikuwa hajui hatua za kuchukua kuokoa wasichana wengine, lakini hivi sasa ameshaokoa zaidi ya wanne.

Alipongeza uamuzi wa shirika kuwakutanisha na wanaharakati nguli katika semina hiyo. Anaamini itawasaidia kupata uzoefu katika kuendeleza jukumu lao la kutetea usawa wa kijinsia.

Msichana Kiongozi kutoka Tabora aliyenufaika na mradi huo, Joyce Agustino alisema mradi huo umemfanya awe imara na kuwa ufahamu mkubwa kuhusu vitu mbalimbali, ikiwamo uchechemuzi, ufeminia na kupingana na mifumo dume.

Alisema wanachofanya katika jamii ni pamoja na kuunganisha wasichana kutoka maeneo mbalimbali na kuwasaidia kutatua changamoto zinazowakabili.

Mkurugenzi wa Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), mmoja wa mwanaharakati, alisema amefurahi kushiriki semina hiyo, akiamini ni fursa kwake kurithisha wasichana hao uzoefu wake.

"Semina hii itazaa matunda. Kwa mfano, mimi katika shirika langu tunapinga rushwa ya ngono. Hivyo, ninapojengea uwezo wasichana, wakaelewa namna bora ya kupambana na rushwa ya ngono, watakuwa na uelewa na baadaye tutapata viongozi wasichana wasio na doa." alisema Janeth.

Kwa mujibu wa TACAIDS, maambukizi mpya kwa watu wazima wenye umri wa kuanzia miaka 15 yamepungua kwa asilimia 16.7 kutoka 72,000 (THIS 2016/17) hadi 60,000 (THIS 2022/23).

Hata hivyo, maambukizi mapya ya VVU yameongezeka maradufu katika kipindi tajwa kwa wasichana wenye umri wa miaka 15-24.

The Guardian

## CAREER OPPORTUNITY

The Guardian Limited, publishers of leading Tanzanian newspapers The Guardian, Nipashe and Nipashe Jumapili, is looking for motivated and experienced professionals to fill the following position:

### Position: Sales Executive

**Job Purposes**
Sales Executive is responsible for driving advertising revenue by selling ad space in our newspapers to businesses, agencies, and other potential clients. This role involves building and maintaining relationships with clients, developing advertising strategies, and achieving sales targets.

**Key Responsibilities**

- Sell advertising space in our newspapers to new and existing clients.
- Develop and implement effective sales strategies to meet or exceed revenue targets.
- Build and maintain strong relationships with clients, understanding their business needs and advertising goals.
- Provide excellent customer service and support to ensure client satisfaction and retention.
- Work with clients to create customized advertising solutions that align with their marketing objectives.
- Stay informed about industry trends, competitor activities, and market conditions.
- Conduct market research to identify potential clients and new business opportunities.
- Maintain accurate records of sales activities, client interactions, and contracts in the CRM system.

**Other Responsibility**

- Develop and guide the team of freelancers.
- Assist and supervise freelancers through post-mortem meetings.
- Accompany freelancers on customer visits, analyze missed business opportunities, and create action plans.
- Monitor and evaluate the performance of freelancers, providing feedback and support for improvement.

**Qualification**

- Bachelor's degree in Marketing, Business Administration, Communications, or a related field.

**Experience:**

- Minimum of 2-3 years of experience in advertising sales, preferably in the media or publishing industry.
- Proven track record of meeting or exceeding sales target

Interested candidates who meet the above criteria should send in their applications enclosing a detailed CV addressed to the:

**HUMAN RESOURCES DEPARTMENT**
**THE GUARDIAN LIMITED**
**P.O.BOX 31042**
**DAR ES SALAAM – TANZANIA**

**OR email: vacancy@guardian.co.tz**
**DEADLINE: 29th June 2024. Only shortlisted candidates will be notified.**

## Migogoro ardhi yaundiwa mkakati

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

WAKAZI wa Kata ya Mapinga, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, mkoani Pwani wameshiriki Operesheni Mapinga inayolenga kutokomeza migogoro ya ardhi.

Operesheni hiyo ya siku tano imeandaliwa na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Mkoa wa Pwani, wataalamu wa sheria na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo.

Akizungumza juzi mjini Mapinga wakati wa operesheni hiyo ambayo kambi yake imewekwa Shule ya Msingi Mapinga, Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Halima Okash alisema wameanzia kata hiyo na baadaye watakwenda Makurunge na Fujayisi.

Alisema kuwa wakati wa operesheni hiyo, watasikiliza na kutatua migogoro ya ardhi katika maeneo husika.

Okash alisema wameona wawawafuate wananchi katika maeneo yao yenye migogoro Ili kutafuta ufumbuzi kwa kushirikiana na wataalamu wa ardhi na wanasheria.

Alisema wapo wananchi wana mashamba makubwa na nyumba nzuri lakini maeneo wanayoishi hawayamiliki kihalali, jambo ambalo ni kinyume cha sheria na taratibu zinavyoelekeza.

"Niwasihi wananchi wafuate utaratibu wa kumilikishwa ardhi isiyo na migogoro na njia sahihi ya kuwa salama ni kufuata taratibu kushirikisha serikali," alisema.

Mkuu wa Wilaya alisema Ili kukabiliana na migogoro hiyo, pia wameanza kubainisha kampuni zinazojihusisha na kupima na kuuza ardhi katika wilaya hiyo kutokana na baadhi ya kampuni kuhusishwa na kuuza maeneo yenye hatimiliki.

Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Dar es Salam na Pwani, Shukrani Kyando alisema ameungana na Mkuu wa Wilaya kusikiliza changamoto za masuala ya ardhi na kuzitafutia ufumbuzi.

Kamishna Kyando alisema kuwa katika operesheni hiyo, wametumia kutoa ushauri kwa kesi ambazo zipo mahakamani wananchi watii amri Ili kupunguza migogoro isiyo ya lazima.

Pia ametoa ushauri kwa wananchi kupima maeneo yao sambamba na kufuata taratibu za umiliki wa ardhi kuepusha migogoro ambayo inatokea kwa kutozingatia taratibu.

Rose Leon, ni mmoja wa wananchi waliojitokeza kushiriki operesheni hiyo, ambaye aliomba serikali kufungia kampuni zinazojihusisha na uuzaji ardhi kutokana na kulalamikiwa kuuza maeneo yenye hatimiliki na kuchangia kuwapo migogoro.

## HABARI KITAIFA



Fundi bomba kutoka Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Hamisi Ayub (kushoto), akiwa kazini kwa ajili ya kutekeleza mradi wa maji katika vijiji vya Mizembwe na Potwe juzi. Wengine ni mafundi wenzake, Mnkai Mhando (kulia), Frank Sechome (wa pili kulia), Fransic Bahari (wa tatu kulia) na (wa nne kulia) ni Peter Fredrick. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# 'Wafoji' namba kuwahi foleni kliniki ya Makonda

**Na Beatrice Shayo,** ARUSHA

BAADHI ya wananchi waliojitokeza katika kliniki ya matibabu katika Jiji la Arusha, wamedaiwa kutumia ujanja wa kutengeneza namba feki ili wapatiwe matibabu kwa haraka.

Tukio hilo limesababisha usumbufu kwa wagonjwa waliochukua namba tangu juzi na kujikuta namba zao zigongana na waliofoji na wao kuanza kuhudumiwa mapema.

Akizungumza jana na wananchi waliojitokeza kwa ajili ya kupatiwa matibabu katika kliniki hiyo ya siku saba, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, alisema wapo ambao walipatiwa namba juzi na hawajapatiwa huduma.

"Kuna watu wamejitengenezea namba zao juzi wamekuja nazo leo (jana) badala ya wale waliobaki juzi kuendelea jana, wakajikuta wamechukuliwa ambao ni wapya, sasa tumekubaliana turejee kwenye namba zilizotolewa juzi," alisema Makonda huku wakimshangilia.

"Lengo ni kuhakikisha wale wote wa juzi ambao wamepatiwa namba wamalizike katika matibabu halafu tuendelee na watu wa leo (jana) tumeelewana?"

Aidha, alisema mpaka sasa madaktari na wauguzi wamefanya kazi kubwa idadi ya watu waliotibiwa imeenda mara tatu ya malengo waliyokuwa nayo.

"Madaktari wamefanya kazi kubwa, wametoka majira ya saa nne usiku na saa 11 alfajiri, wapo katika hivi viwanja. Ninaomba niwahakikishie wananchi wote wa Mkoa wa Arusha hakuna atakayekanyaga katika hivi viwanja asipatiwe matibabu.



"Usijisikie vibaya ukadhani kuna mtu amechukua nafasi yako haya mambo ya kuwahi na kuchukua namba ya mtu mwingine unaweza kupata ugonjwa ambao si wako ila si tabia njema kutengeneza namba bandia kutaka kuwahi jambo ambalo muda wako haujafika.

"Tuna hadi miwani tunayotoa bure, gharama yake ni Sh. milioni moja, nimefurahi kuona yule bibi alivyopatiwa miwani alikuwa anafurahia, naombeni mjitokeze pia kuna saratani ya tezi dume, nenda ukapime bure, hii fursa usiiache," alisema.

Makonda alisema kuna baadhi wakienda kupima hospitali wanajikuta tatizo lao limefika kwenye hatua mbaya wakati angewahi kupima afya angegundulika mapema.

Aidha, alisema tayari kuna wadau wamejitolea dawa za Sh. milioni 25, Bohari ya Dawa (MSD) wametoa dawa za Sh. milioni 12 na kama kuna wengine wapo tayari kuchangia dawa na vifaa wanakaribishwa.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Dk. Charles Mkombachepa, alisema mwitikio wa wagonjwa waliojitokeza ni mkubwa na wanaendelea kuwahudumia.

Alisema wagonjwa wengi wapo katika magonjwa ya ndani, huduma ya macho, kupima kifua kikuu, huduma za saratani.

Alisema huduma za rufani wanazitoa kwa haraka na kupatiwa matibabu katika hospitali za serikali na binafsi.

Dk. Mkombacheka alisema juzi walihudumia wagonjwa 2,034. Kati yao, wanawake 1,053 na wanaume 973.

### WALALAMIKIA KUKOSA DAWA

Elizabeth Bosco, aliyefanyiwa vipimo, amelalamikia kitendo cha kupewa dawa za siku tatu badala ya siku 14.

"Nimepewa dawa nusu naambiwa dawa zimeisha sasa hizo za siku nyingine nitazipata wapi wakati sina hela ya kwenda kuzinunua hizi dawa?" alihoji.

Jack Amfrey alisema mtoto wake amebainika ana tatizo kiafya na kuandikiwa dawa za aina mbili ambazo ametakiwa kwenda kuzinunua kwa kuwa dawa zimeisha.

Mahema yenye foleni kubwa ni ya Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), hema la kuhudumia watoto, saratani, magonjwa ya ndani na huduma ya macho.

# Watu watatu wa familia moja wafa wakitoka harusini

**Na Oscar Assenga,** KOROGWE

WANAFAMILIA watatu waliokuwa wakitoka katika harusi ya kijana wao jijini Dar es Salaam kurejea Rombo, mkoani Kilimanjaro, wamepoteza maisha kwa ajali baada ya gari waliokuwa wanatumia, kuacha njia na kupinduka.

Waliofariki dunia katika ajali hiyo iliyotokea juzi alfajiri eneo la Bwiko, Wilaya ya Korogwe, mkoani Tanga, ni mama wa bwana harusi, dada mkubwa wa familia ya bwana harusi na shangazi yake huku watu wengine wanne wakijeruhiwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Almachius Mchunguzi, alithibitisha jana kutokea ajali hiyo na kueleza kwamba wanafamilia hao walikuwa katika gari dogo aina ya Toyota Noah lenye namba za usajili T 979 CZM.

"Ni kweli hao watu walikuwa wakitokea harusini Dar es Salaam kuelekea Wilaya ya Rombo (Kilimanjaro), ambapo walipofika Bwiko, gari lao lililokuwa likiendeshwa na Godfrey Michael (34), ghafla liliacha njia kwenda porini na kupinduka," alisema.

Kamanda Mchunguzi aliwataja marehemu hao ni Cecilia Luka, maarufu Kamashu (58), Judith Juma (42), wote wakazi wa Rombo na mwingine alifariki dunia baada ya kufikishwa eneo la mapokezi ya Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga (Bombo).

Kiongozi huyo wa Jeshi la Polisi alisema kuwa majeruhi waliokimbizwa Hospitali ya Bombo kwa ajili ya kupata matibabu walikuwa wanne.

Aliwataja majeruhi hao ni Joshua Michael (27), mfanyabiashara, Jackline Masawe (32), Antonio Luka (40) na mwingine aliyetambuliwa kwa jina moja la Carene, wote wakazi wa Rombo.

Alisema majeruhi hao awali walipatiwa matibabu katika Kituo cha Afya Mombo kabla ya kuhamishiwa Bombo kwa matibabu zaidi.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga (Bombo), Dk. Frank Shega, alisema kuwa Juni 24 mwaka huu, jioni walipokea majeruhi wanne wa ajali hiyo na wakati wakiwa mapokezi mmoja aliyekuwa na hali mbaya alifariki dunia kabla ya kufika wodini.

Kwa mujibu wa Dk. Shega, waliwapokea majeruhi ambao ni mtoto mmoja (15) na watu wazima watatu.

Alisema kwamba aliyefariki dunia wakati akipokewa mapokezi alikuwa ameumia sehemu ya kichwa na tumboni na alikuwa na mivunjiko mingi.

Dk. Shega, alisema kuwa kutokana na hali zao kuwa mbaya, mmoja ameshapewa rufani kwenda Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kaskazini (KCMC), Moshi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Turasimishe biashara, tusinyanyaswe masoko ya kimataifa

**MACHI** 21, 2018, nchi za Afrika zilisaini mkataba wa makubaliano ya Eneo Huru la Biashara (AfCFTA), ambalo linakadiriwa kuwa na watu zaidi ya bilioni 1.2 na pato la dola za Marekani trilioni 2.5 kwa mwaka.

Vipo vigezo ambavyo vitawawezesha wafanyabiashara wa Tanzania kulifikia soko hilo na masoko mengine ya kimataifa ambayo yanaruhusu nchi nyingine kuuza huduma na bidhaa zake nchini.

Moja ya kigezo ni kuwa na biashara iliyosajiliwa ambayo inatunza kumbukumbu zake za kifedha, mauzo, ununuzi, uzalishaji (kwa wenye viwanda), na namna wafanyabiashara wanavyozingatia ajenda ya dunia ya maendeleo endelevu kwa sekta zote.

Hapa nchini, zipo mamlaka na taasisi zinazoratibisha masuala ya biashara na kuthibitisha uhalali wake, ambazo ni muhimu wananchi wazitumie kikamilifu ili AfCFTA na masoko mengine yawanufaishe Watanzania.

Moja ya taasisi hiyo ni Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), ambayo inasajili kampuni, majina ya biashara, nembo za biashara, leseni za viwanda, miliki ubunifu na uvumbuzi (hataza).

Takwimu za BRELA zinaonyesha kwamba ni Watanzania wachache wanaomiliki biashara changa, ndogo na za kati wanaoona umuhimu wa kuzisajili. Kibaya zaidi ni kwamba ni wavumbuzi wachache zaidi, wanaojisajili kwa wakala huo.

Jambo la kusikitisha ni kwamba gharama za kujisajili zinahimilika ukilinganisha na hasara ambayo mtu anaweza kuipata kwa kutoilinda biashara yake kisheria.

Mathalani, kiwanda kidogo chenye mtaji wa chini ya Sh. milioni 10, kinachosindika unga, viungo au kinazalisha mafuta kinasajiliwa kwa Sh. 50,000 inayolipwa mara moja tu katika uhai wake wote.

Kwa wavumbuzi, ada ni Sh. 22,000 inayolipwa kwa awamu mbili na Sh. 4,000 kila mwaka baada ya kusajiliwa. Hiki ni kiasi kidogo ambacho bila shaka, Mtanzania mwenye nia ya kufanyabiashara kwa uaminifu, anamudu kuilipa.

Kama tunavyofahamu, mazingira ya Afrika kwa maana ya changamoto zinazoikabili jamii zinafanana kwa kiasi kikubwa; inasikitisha kuona mtu anabuni kitu kinachoweza kutatua changamoto kwenye jamii, anakiweka mtandaoni, anakipa na jina, bila kulinda jina wala uvumbuzi wenyewe.

Hali ni hiyo hiyo wakati wa maonyesho ya biashara kama ya Kimataifa ya Sabasaba ambayo yako mbioni kuanza; unakuta mbunifu anaeleza hatua kwa hatua namna alivyofanikiwa kubuni zana fulani ya kuwasaidia wakulima au wananchi katika sekta muhimu, baada ya maonyesho hanufaiki na ubunifu wake kwa kuwa wajanja wachache wanaamua kwenda kuisajili BRELA na kuanza kuizalisha. Hii ni hasara sio kwake pekee bali kwa nchi pia.

Mpango wa serikali wa kuboresha mazingira ya biashara nchini umeweka njia rahisi za kujisajili ambayo ni kupitia mtandao (ORS), unapata huduma zote za kurasimisha biashara yako ukiwa sehemu yoyote yenye intaneti.


Tunaeleza haya ili kuukumbusha umma kwamba wajasiriamali wetu wanaweza kuzalisha bidhaa nzuri, kutoa huduma bora, tukajitangaza mtandaoni lakini mwisho wa siku, tutakuta kile tunachouza kimelindwa kisheria na mtu mwingine; ambaye atakuruhusu kuendelea kutumia nembo au jina ulilobuni, kwa kumlipa mamilioni ya fedha kwa kuwa tu ameshajisajili.

Sheria itamlinda ambaye ameitii. Hata kama utakuwa mwanzishili wa huduma, jina, uvumbuzi au nembo, usipoisajili halafu akatokea mgeni akaisajili nchini, hutaweza kujitetea kwa sababu hutambuliki kwenye mifumo ya kisheria.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




Na Joyce Lameck

## Muungwana Lazima Nilonge

# Kamari dubwi inaharibu watoto

**KWANGU** ni ajabu kumkuta mtoto badala ya kuwa shuleni, anazagaa kama kondoo asiye na mchungaji, akiwa sehemu ya kundi la wanaocheza mchezo wa kubashiri wa dubwi mitaani.

Tena bila shaka wala wasiwasi akiwa makini na kile anachokifanya akidhani kuwa ni sahihi, hata bila kujali kuwa ana umri mdogo na tena alitakiwa kuwa darasani akisoma

Yamejengeka mazoea kwa watoto kujihusisha na mchezo wa dubwi , wenye majina kama ' Mchina, dubwika, korokoro' .

Maeneo mengi mijini hasa miji mikuu ni mambo ya kawaida kutokana na kuzungukwa na madubwi kila mahali.

Ukiwasikiliza wana jamii, wanaozungumza na gazeti hili wanakuambia ni ngumu kumzuia mtoto kushiriki kucheza mchezo huo kwani umewekwa karibu na nyumba zao na unawavuta walio wengi.

Wazazi na walezi nao wanashindwa kujenga ukaribu na watoto wao kutokana na kuhangaika na maisha na kukosa muda wa kukaa nao kujenga ukaribu na urafiki pia kufahamu na kutatua changamoto za nyumbani na shuleni.

Watoto chini ya miaka 18 hawaruhusiwi kushiriki kucheza kamari wala kunywa pombe, kama ilivyo kwenye mambo mengine ambayo hayaruhusiwi kwa watoto kutokana na athari watakazozipta kulingana na umri wao mdogo.

Ukichunguza wakati mwingine unagundua wanacheza kupitia watu wazima kwa lengo kuwa kama akipata ushindi kutokana na pesa alizompa wagawane.

Watu wazima huenda jamaa zao au marafiki hupokea pesa za watoto bila kujali ni njia zipi mtoto amezipata.

Mfano, kachukua fedha za nauli ya shule, kaiba au za kununulia mahitaji nyumbani. Ni wazi kuwa hana kazi yoyote ambayo inamwingizia kipato, inakuwaje upokee fedha yake?.

Dubwi linawalazimisha watoto kutumia njia zisizo sahihi katika kujipatia fedha, kwajili ya kuchezeasha mchezo huo wa kamari bila mzazi au mlezi kufamu.

Ikumbukwe hii inaweza kusababishia mtoto kuingia kwenye makundi hatarishi ya kihalifu ya wezi, waporaji na hata kuwa tapeli kwa kwasababu ya kupata fedha kufanikisha mchezo wake.

Inavyoelekea michezo hii ya dubwi haijajumuishwa kwenye udhibiti, hali hiyo imefanya iwe na uhuru wa kuweka mashine zake kila sehemu hata vijijini ambapo watu wanacheza bila hofu.

Inavyoonekana wengine wana uraibu wa michezo hiyo, ndiyo maana mtoto anaacha kwenda shule akiendelea kucheza kamari baa.

Serikali itazame mchezo wa dubwi upatikane sehemu za starehe zenye udhibiti maalum na si kuacha mambo kiholela , ili kuzuia madhara ambayo yatawapata watoto hasa kushindwa shule.

Kuna madai kuwa ni mchezo iliyopewa uhuru inahitaji kutazamwa kama ilivyo pombe na vitu vingine ambavyo vimetengwa na watoto, ili kuwadhibiti wasiwe sehemu ya wateja wa mambo yaliyo juu ya uwezo wao.

Ni lazima kuwalinda na kuweka jitihada katika masomo kwa ajili ya maisha yao ya badaye kwani michezo hii inawapotezea muda na kuwaingiza kwenye uhalifu na kamari utotoni.

Taratibu za makorokoro zinapaswa kupitiwa upya na kudhibitiwa ili kuzia watoto wasitoroke shuleni na kwenda kucheza lakini pia ziwekwe sheria ambazo zitafanya mchezo huo upatikane sehemu maalumu si kila baa wala mgahawa.

Ni wakati wa kuweke tamko la kuboresha michezo hiyo hadharani kuwa ni marufuku kuhusisha watoto na kuwe na ufuatiliaji hasa kwenye baa, vilabu vya pombe na kwenye maneo ya burudani mitaani.

Mzigo usiwe kwa mwenye mchezo pekee au mmiliki wa baa kwamba asiruhusu watoto wacheze au muda wa kucheza, bali iwe ni kila mmoja kusimamia.

Hasa eneo ambalo mchezo upo na kuhoji kuna kibali cha kumiliki au kuna tahadhari za kusimamia wachezaji.

Ni suala ambalo kila mzazi na mlezi anapaswa kulichukulia kwa uzito na kuweka mkazo katika malezi ya mtoto.

Ni vema serikali kuchukua hatua juu ya suala hili kwa haraka, ili kupata ufumbuzi wa jambo hili ili kulinda kundi kubwa la watoto ambao tayari wameshaingia kwenye michezo wa dubwi na wale ambao hawajaushiriki.

## HABARI KITAIFA



Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Tanga, Rajabu Abdallah (kulia), akikabidhi fulana za chama hicho kwa Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Muheza, Laick Gugu, wakati wa mkutano wa Halmashauri Kuu ya CCM ya wilaya hiyo, juzi. Kushoto Katibu wa chama hicho wa wilaya hiyo, Simon Leng'ese. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Matumizi holela dawa za maumivu tishio

**Na Christina Mwakangale**

WATAALAMU wa afya wamesema matumizi ya dawa za kutuliza maumivu yameshika kasi kwa vijana, hasa wanafunzi nchini, kinyume cha mwongozo wa kitabibu.

Aidha, ongezeko kubwa la waraibu wa dawa hizo ni wanafunzi ambao hutumia kwa ajili ya starehe.

Miongoni mwa dawa hizo ni tramadol au valium, ambazo hutolewa kwa mgonjwa mwenye maumivu ya muda au kudumu baada ya upasuaji au selimundu.

Mfamasia kutoka Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe (MNMHH), Steward Ngangaje, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki katika mada: Uraibu wa Dawa za Kulevya kwa Vijana; Madhara na Matibabu, iliyoandaliwa na hospitali hiyo kupitia mtandao wa X.

"Dawa za kulevya ni kemikali ambazo huingia katika ubongo na kumwathiri mtumiaji, kusababisha fikra, hisia, kuleta matendo tofauti kwa matarajio ya umma. Wapo ambao hutumia dawa za kulevya kwa njia ya kula/kunywa, kuvuta au kujidunga.

Alisema ingawa zipo dawa za aina hiyo ambazo lengo lake ni kwa ajili ya kutumika kwa ambaye ana maumivu makali au ana ugonjwa sugu, utumiaji kwa zaidi ya siku 14 huwa ni uraibu.

"Zipo dawa ambazo zimeruhusiwa kisheria na kutoa maelekezo, kama pombe, tumbaku. Mfano shisha inatumika kwa kuweka tumbaku na si kama ilivyo sasa baadhi huweka bangi, tramadol, heroin, tunazo taarifa kutoka tunaowatibu kituoni kwetu.

Mirungi, cocaine nazo hutumika. Hospitalini kuna dawa ambazo mtu anaandikiwa kutokana na changamoto ya maumivu kwa muda mrefu. Matumizi ya muda mrefu kama wiki mbili, dawa kama valium, tramadol ni uraibu. Zimeruhusiwa kutumika kwa utaratibu, lakini nje ya utaratibu zinaweza kuleta uraibu," alifafanua Steward.

Alitaja sababu saba za vijana kutumia dawa hizo ni, kuiga tabia katika kundi rika, kukosa shughuli za kufanya, magonjwa ya akili kama msongo wa mawazo.

Zingine ni vijana kujiingiza katika starehe kama klabu za usiku, mila na desturi, teknolojia na usasa, malezi duni kutoka kwa walezi na wazazi kwa watoto wao, akisema baadhi yaoo waliopo kituoni hapo wanaofikia 617 hutoa sababu tofauti.

"Ukimuuliza kwa nini uliamua kutumia dawa za kulevya kama bangi, anasema baba aliachana na mama au natumia heroin baba alikuwa hanipendi. Ama wakati mwingine maradhi ni sababu, anayeumwa selimundu anapewa dawa kama tramadol apunguze maumivu, akitumia sana ni uraibu," alisema.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, asilimia 80 hadi 90 ya wenye uraibu ambayo takribani 617 wengi wao ni umri kuanzia miaka 16 hadi 40. Asilimia 50 walianza dawa za kulevya wakiwa shule ya msingi, sekondari, wachache wakiwa kazini.

Kaimu Kamishna Msaidizi wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Kanda ya Kati, Christian Mbwasi, amesema matumizi ya dawa hizo yanaathari za kidiplomasia, kiuchumi, kiafya, kijamii, kisiasa na kimazingira, akizitaja kuwa ni pamoja na kuhudhuria kliniki za methadone na ushauri kisaikolojia.

Alisema matumizi ya dawa za kutuliza maumivu yameongezeka huku utumiaji wake ukichepushwa kugeuka chanzo cha starehe, kuliko ilivyo usahihi wake dawa imsaidie mgonjwa.

**TIBA**

Msaikolojia kutoka MNMHH, Dk. Swai Japhet, amesema hutoa tiba kwa kutumia maongezi na mwathiriwa kwa kumtengeneza upya mtumiaji wa dawa hizo, ili awe na fikra mpya kichwani mwake.

Tiba nyingine ni kuwapa uhamasishaji wa mafanikio kwa kuwapa mbinu tofauti na kuyafikia malengo na kufanikiwa ili kuachana na fikra hasi kwenye ubongo wake.

"Wanaoacha ghafla huwa na kiu fulani inayomsukuma, tunatumia tiba ya kisaikolojia kumbadilisha. Nashauri walezi wa vituo vya MAT wawe waadilifu. Wanasaikolojia huwa hatusemi moja kwa moja aache, tunashughulika na akili yake.

"Wazazi wengi hadi kutufikia wanasaikolojia huwa wamezunguka sana, wengine husema ni mapepo. Unyanyapaa, hufanya wawalete vijana kwetu wakiwa tayari wamefikia hatua mbaya, tangu wakiwa umri wa kupevuka tukiwapata elimu mapema tutawaelimisha wakabadilika kuliko kuleta mtu mzima ana zaidi ya miaka 30."

Nchini Vituo vya Tiba Saidizi kwa Kutumia Dawa (Medically Assisted Therapy-MAT, vimefikia 16, kikiwamo kilichopo Gereza la Segerea.

Kabla ya kliniki ya MAT, kuanzishwa nchini, kulikuwa ongezeko la Watu Wanaojidunga Dawa za Kulevya (PWID), 50,000 huku wakijuhusisha na kuchangia sindano na kushiriki ngono bila kinga.

Takwimu zikionesha PWID kwa asilimia 28 ya waliojidunga ni wa kiume na asilimia 62 ni wa kike. Kwa mujibu wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Vituo vya MAT vilivyopo nchini ni MNH; Hospitali ya Rufani ya Mkoa Mwananyamala; Hospitali ya Rufani ya Mkoa Temeke; Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya (MZRH), Hospitali ya Sekou Toure, Mwanza; MNMHH, Dodoma; Hospitali ya Bagamoyo, Pwani; Hospitali ya Bombo, Tanga.

Vituo vingine Hospitali ya Tumbi, Pwani; Hospitali ya Mount Meru, Arusha; Kituo cha Afya Tunduma, Songwe na Gereza la Segerea; Kituo cha Afya Tegeta; Zahanati ya Mbagala; Hospitali ya Kigamboni mkoani Dar es Salaam.

## KABWELA

**Na Fadhil Mohammed**



HABARI KITAIFA

# Wajasiriamali EOTF wauza bidhaa za tril. 1/- miaka 27

**Na Joseph Mwendapole**

WAJASIRIAMALI wanaofadhiliwa na Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote (EOTF), wameuza bidhaa ndani na nje ya nchi zenye thamani ya Sh. trilioni moja kwa miaka 27 tangu mfuko ulipoanzishwa.

Mwenyekiti wa Mfuko huo, Anna Mkapa, aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam, wakati wa mafunzo ya 27 ya biashara ya wajasiriamali wanawake kutoka Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara.

Alishukuru wafadhili waliowezesha mafunzo hayo ambayo yamekuwa na manufaa makubwa kwa wanawake wajasiriamali nchini.

Alisema tangu kuanzishwa kwa EOTF, wametoa mafunzo kama hayo yanayowajenga uwezo na stadi za biashara maelfu ya wanawake wajasiriamali nchini.

Alisema mafunzo hayo yalianza miaka 27 iliyopita na huwa yanafanyika kila mwezi Juni, kuwawezesha wanawake kufanyabiashara na kushiriki maonesho ndani na nje ya nchi ili wapate uzoefu wa biashara.

Mkapa alisema tangu mafunzo hayo yaanze mwaka 1997, wanawake wajasiriamali milioni sita wameshafikiwa na kunufaika na mafunzo hayo na wameanzisha biashara ambazo zimestawi.

"Maelfu ya wanawake wamekuwa wakipata fursa za masoko ya ndani na nje ya nchi na kwa muda wote huo, wamefanikiwa kuuza ndani na nje ya nchi bidhaa zenye thamani ya trilioni moja," alisema.

Alisema taasisi hiyo inakabiliana na changamoto ya fedha za kuwahudumia wanawake wajasiriamali, kutokana na wengi wao kuhitaji mafunzo hayo ili waweze kukuza biashara.

"Ninaawashukuru sana wafadhili waliofanikisha mafunzo haya kwa sababu wanawake wanahitaji kushikwa mkono ili kujikwamua katika umaskini kwa kufanya biashara zenye ubora kitaifa na kimataifa," alisema.

Alisema EOTF inahitaji kuanzisha kanda inazozihudumia ili iwe rahisi kwake kuwafikia wananchi wengi na kuwapa mafunzo kama hayo ambayo yamewakwamua wanawake wengi.

"Kuna changamoto kubwa ya gharama za kushiriki maonyesho ya biashara kila mwaka kwasababu EOTF ni mhamasishaji tu na sio mfanyabiashara, kwahiyo tunaomba Wizara ya Viwanda itoe msamaha ili wajasiriamali waweze kushiriki maonyesho na kupata uzoefu wa biashara," alisema.

Mkurugenzi wa Usimamizi wa Biashara wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (Tantrade), Crispin Luanda, aliipongeza EOTF kwa kuwezesha wanawake wajasiriamali kupata mafunzo kwa miaka yote 27 tangu kuanzishwa kwake.

Alishukuru wafadhili wa EOTF ambao wamekuwa wakiiwezesha taasisi hiyo kiuchumi ili kuwapa mafunzo wajasiriamali wanawake na kuchangia mafanikio makubwa yaliyopatikana.

"Mafunzo haya ni muhimu na msingi mzuri kwa mfanyabiashara mdogo kwani anapata elimu ya kutafuta masoko, kutunza fedha na namna ya kuendesha biashara yake," alisema.

Aliishauri EOTF kuwapa mafunzo pia, wajasiriamali hao ya namna ya kufanyabiashara kidijitali zaidi ili waweze kuyafikia masoko mengi na kwa gharama nafuu badala ya kubaki na mtindo ule ule wa maisha.

"Tutumie simu janja kufanyabiashara kwa namna ya kisasa kwasababu biashara nyingi kwa sasa biashara ziko kidijitali ukiwa hapa nchini unaweza kufanya biashara popote pale kwa hiyo twende na wakati," alisema.

Luanda alisema TANTRADE imechukua maombi ya EOTF ya kutaka kupewa unafuu wa kushiriki maonyesho ya biashara ya kimataifa ili kuwapa fursa wanawake wengi wa maeneo ya vijijini kushiriki maonyesho hayo.

"Tumshukuru sana Mama Anna Mkapa kwasababu pamoja na changamoto zote ambazo EOTF inapitia, lakini kila mwaka anaandaa mafunzo kama haya. Sisi Tantrade tunamuunga mkono na tutaendelea kumuunga mkono siku zote," alisema.

Mmoja wa wajasirisiamali hao, Happyness Maiko, alisema alianza kupata mafunzo hayo mwaka 2018 na hadi sasa biashara yake ya mafuta ya alizeti imesimama vizuri na amefanikiwa kuanzisha kiwanda kidogo nyumbani kwake Mikocheni kinachotengeneza bidhaa na kuuza mikoa mbalimbali.






## 'Wasafirishaji wapewe elimu biashara haramu ya viumbepori'

**Na Jenifer Gilla**

BARAZA la Wasafirishaji Shehena Tanzania limesema elimu ya biashara haramu ya viumbepori inapaswa kutolewa mara kwa mara kwa wasafirishaji ili kuwaongezea umakini katika kudhibiti usafirishaji bidhaa hizo na kumaliza tatizo hilo.

Mwenyekiti wa Baraza hilo, Clement Kamendu, aliyasema hayo mwanzoni mwa wiki wakati akichangia mdahalo uliohusu ushirikishwaji sekta binafsi katika kutokomeza biashara haramu ya viumbepori ulioandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira nchini (JET).

Alisema ingawa serikali imefanikiwa kudhibiti biashara hiyo kwa kiasi kikubwa, bado inafanyika kwa siri.

Alisema elimu ikiwa endelevu kwa wasafirishaji itasaidia kuwafanya wawe macho muda wote kutambua mizigo haramu na wasafirishaji wake.

Kamendu alisema tani bilioni 12 za shehena zinasafirishwa kila mwaka duniani na kati ya hizo, hakukosekani shehena za biashara haramu ambazo zimepita ama kwa kushirikiana au kutoshirikiana na wasafirishaji.

Alisema katika kupambana na biashara hiyo, baraza hilo kwa kushirikiana na wadau ikiwamo USAID-Tuhifadhi Maliasili na Jeshi la Polisi, wanatoa mafunzo kwa wasafirishaji wote wakiwamo wa mabasi, ndege na magari ya mizigo, ili kujenga weledi na umakini katika kazi zao.

Alisema moja ya elimu wanayowapatia ni namna ya kuvitambua viashiria vya kupitisha mzigo haramu, akitaja kimojawapo kuwa ni wasafirishaji hawalipi fedha kwa njia ya kielektroniki wakiepuka kuacha alama.

Kadhalika alisema hupeleka mizigo muda wa kukaribia kufunga ofisi wakiamini wahusika wanakuwa wamechoka na umakini kupungua.

Mkuu wa Kitengo cha Sera wa Mradi wa USAID-Tuhifadhi Maliasili, Allen Mgaza, alisema ingawa serikali imedhibiti biashara hiyo kwa kiasi kikubwa, lakini kunahitajika kuongeza nguvu hasa katika elimu ya uhifadhi ili kuitokomeza kabisa.

Alisema ili kuongeza nguvu katika kudhibiti ni lazima kuwapo na ujumuishi wa serikali na sekta binafsi kwa sababu majangili wanatekeleza kazi hiyo kwa kushirikiana na wengine na kutengeneza mitandao na madhara huwapata sekta zote.

Alisema biashara hiyo ina madhara makubwa kwa taifa ikiwamo kusababisha rasilimali kutoweka kwa sababu haifanyiki kwa njia salama na endelevu na kuchochea matendo mengine ya kihalifu.

Alisema pia husababisha taifa kupoteza rasilimali muhimu za utalii kwa kuwa vivutio vya utalii vitapungua, hivyo kukosa mapato yatokanayo na utalii.

Mkurugenzi wa JET, John Chikomo, alisema wanashiriki kudhibiti biashara hiyo kwa kuwajengea waandishi wa habari uwezo kuhusu uhifadhi wa viumbepori ili waandike habari zenye kuleta uchechemuzi kwa jamii.



# Afungwa jela miaka mitatu kwa udanganyifu mitihani

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Babati, mkoani Manyara, imewahukumu watu wawili kutumikia kifungo cha miaka mitatu jela kila mmoja, baada ya kutiwa hatiani kwa kosa la kufanya udanganyifu wa kuwafanyia mitihani ya taifa wanafunzi wa kidato cha nne na kughushi nyaraka.

Waliohukumiwa adhabu hiyo, ni Jacob Dezderi (21), Mkazi wa Bashneti, Wilaya ya Babati na Paschal Sikai (33), Mkazi wa Dareda, ambaye alikuwa Mwalimu wa kujitolea.

Akisoma hukumu hiyo jana, Hakimu Mfawidhi Mwandamizi wa Mahakama hiyo, Victor Kimario, alisema mahakama hiyo imejiridhisha kwamba washtakiwa hao walifanya udanganyifu huo mwaka 2023, kwa kuwafanyia mitihani wanafunzi wa kujitegemea, kisha kughushi nyaraka za barua ya utambulisho wa kufanyia mitihani.

Kwa mujibu wa hakimu Kimario, makosa hayo walifanya Novemba 13 na 14 mwaka jana.

Alisema washtakiwa walikamatwa Novemba 14 mwaka 2023, baada ya kukiuka Sheria ya Baraza la Mitihani la Tanzania, Kifungu cha 19 (a) na Kifungu 24 (1), Sura 107 iliyofanyiwa Marejeo Mwaka 2019.

Washtakiwa hao kwa pamoja walikiuka matakwa ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Kifungu cha 333, 335 (a) na 337, Sura ya 16, iliyofanyiwa Marejeo ya Mwaka 2022.

Aidha, Hakimu Kimario, alisema mshtakiwa namba moja, alijifanya kuwa anaitwa Daudi Buxay, na mshtakiwa wa pili, alijiita Isaya Mtinda na wote walikuwa wakiwafanyia mitihani watahiniwa wa kujitegemea katika Shule ya Sekondari Endamanang,' na walinaswa wakiwa kwenye mtihani wa Hisabati huku wakiwa tayari walishafanya mitihani ya Uraia na Kingereza.

Alisema mahakama ilipomhoji mshtakiwa namba moja, Jacob Dezderi, alidai kuwa aliitwa kutoka Mbeya, kwa ajili ya kazi maalum, ila hakuithibitishia mahakama ni kazi gani, huku mshtakiwa wa pili, akikana mbele ya mahakama kuwa hakuwapo.

Akisoma hukumu hiyo, hakimu Kimario alisema kitendo walichokifanya siyo hasara kwao au kwa wateja wao bali ni hasara kwa taifa na jamii kwa ujumla, kwa kusababisha madhara ambayo pengine yanaweza kuligharimu taifa kwamba kama ni daktari anaweza kudunga mgonjwa sindano kumbe hakustahili.

Awali, Wakili wa Serikali, Leonce Bizimana, alidai mahakamani hapo kwamba kosa walilolifanya la udanganyifu wa kuwafanyia mitihani watu wengine, lina athari hasi katika taifa.

## RC aagiza msako watuhumiwa wa ulawiti, ubakaji watoto

**Na Steven William,** MUHEZA

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dk. Batilda Buriani, ameagiza kufanyika msako maalum usiku na mchana wa kuwatafuta watuhumiwa wa ubakaji na ulawiti, waliowafanyia watoto wanane kwa kuwarubuni wakiwa kwenye kibanda cha kukaangia mihogo.

Watoto hao wanadaiwa kubakwa na kulawitiwa, wakiwa jirani na shule yao iliyoko Wilaya ya Handeni, mkoani Tanga.

Alitoa agizo hilo juzi, alipokwenda kuzungumza na madiwani wa Wilaya ya Muheza, waliokuwa wakiendelea na kikao maalumu cha baraza la madiwani, lililoketi kupokea taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Pamoja na mambo mengine, alilaani kitendo hicho na kuagiza kufanyika kwa kura za siri, ili kubaini watu wote wanaounga mkono vitendo hivyo.

Pia, alilitaka Jeshi la Polisi mkoani hapa kutolala na wajitume kuwasaka watuhumiwa hao hadi wapatikane katika kipindi cha muda mfupi kuanzia sasa. Vilevile, alisema kitendo cha aina hiyo pia kimeripotiwa katika Wilaya ya Mkinga, huku akiitaka jamii kufunga kibwebwe kupambana na vitendo hivyo, kwa kuwa kama vikiachwa vinaweza kuathiri kizazi cha sasa na baadaye.

Balozi Dk. Burian, alisema kuwa iwapo uchunguzi utafanyika na akapatikana mtu yeyote, awe mwalimu au kiongozi wa dini yeyote, hawatamwacha kwani vitendo hivyo vimekuwa vikidhoofisha nguvu kazi ya taifa.

Alisema: "Watu wazima wameanzisha kigenge cha makusudi cha danganya toto, kumbe wana shughuli zao nyingine watoto wakienda wanadanganywa na mihogo ya kukaanga, wanawadhulumu watoto wadogo wa kike wa miaka 8, 9 mpaka 10. Huyo wa mwisho aliendа akapatwa na changamoto ya kutokwa na damu nyingi kwa kuwa alikuwa ni mdogo ndiyo watu wakajua".

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya kifungu cha 19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania na Kanuni ya 20 (4) ya Kanuni za Mafuta Biashara ya Jumla, Uhifadhi, Rejareja na Matumizi Binafsi), Gazeti la Serikali Toleo Na. 150 la 2022)**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya kubadili umiliki wa leseni na jina la kituo cha mafuta kama ifuatavyo: -

| | |
|---|---|
| **Jina la awali la kituo:** | Jonas N. Nyagawa – J. N. Petrol Station |
| **Nambari ya Leseni:** | PRL-2021-073 |
| **Mahali Kituo kilipo:** | Kiwanja Na. 125, Kitalu 'E', Kitwiru, Manispaa ya Iringa, Mkoa wa Iringa |
| **Jina linalopendekezwa:** | Manyanya's Oil Limited |
| **Mmiliki wa awali:** | Jonas N. Nyagawa |
| **Mmiliki mpya:** | Manyanya's Oil Limited |

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya mabadiliko ya umiliki na majina ya leseni tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne tokea tarehe ya tangazo hili.

**EWURA House, 3 EWURA Street, 41104 Tambukareli,P.O Box 2857, Dodoma**
**Tel: +255-26 2329003-3; Fax: +255-26 2329005; , Toll-Free 0800110030**
**Email: info@ewura.go.tz Website: www.ewura.go.tz**

**Imetolewa na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

TAARIFA KWA UMMA

(Imetolewa chini ya kifungu cha 19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania na Kanuni ya 20 (4) ya Kanuni za Mafuta Biashara ya Jumla, Uhifadhi, Rejareja na Matumizi Binafsi), Gazeti la Serikali Toleo Na. 150 la 2022)

TAARIFA inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya kubadili umiliki wa leseni na jina la kituo cha mafuta kama ifuatavyo: -

| | |
|---|---|
| **Jina la awali la kituo:** | Blue Coast Investment Limited |
| **Nambari ya Leseni:** | PRL-2023-236 |
| **Mahali Kituo kilipo:** | Kiwanja Na. 176, Kitalu "E", Eneo la Ihayabuyaga, Geita Mjini, Wilaya ya Geita, Mkoa wa Geita |
| **Jina linalopendekezwa:** | Blue Coast Energy (T) Limited |
| **Mmiliki wa awali:** | Blue Coast Investment Limited |
| **Mmiliki mpya:** | Blue Coast Energy (T) Limited |

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya mabadiliko ya umiliki na majina ya leseni tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne tokea tarehe ya tangazo hili.

**EWURA House, 3 EWURA Street, 41104 Tambukareli, P.O Box 2857, Dodoma**
**Tel: +255-26 2329003-3; Fax: +255-26 2329005;**
**Toll-Free 0800110030, Email: info@ewura.go.tz Website: www.ewura.go.tz**

Imetolewa na:
Mkurugenzi Mkuu
EWURA



# Shule binafsi, umma zaonywa mabasi mabovu

**Na Rose Jacob,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza limewaonya wamiliki wa shule binafsi na za serikali kuacha kutumia magari mabovu yanayotoa huduma za usafiri kwa wanafunzi.

Bali limewataka wazingitie maeneo saba katika kuhakikisha usalama wa watu na kuepuka ajali za mara kwa mara.

Akizungumza katika uzinduzi wa kampeni ya ukaguzi wa magari yanayotoa huduma za usafirishaji kwa wanafunzi katika shule za umma na binafsi jijini hapa, Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Mwanza, Wilbroad Mutafungwa, aliwataka wakaguzi wa magari hayo kuzingatia mambo kadhaa ikiwemo uchakavu wa bodi la gari.

Pia, aliwataka kuzingatia uchakavu wa matairi, uwepo wa mikanda kwenye viti vya abiria, taa, leseni ya dereva, umahiri na ufanisi wa dereva ikiwemo uoni wa dereva na uwepo wa mwangalizi wa wanafunzi katika gari husika.

"Kuna mifano ya ajali mbaya za barabarani hasa kwa magari ya shule zilizosababisha vifo vya wanafunzi, uchunguzi ukifanyika unaonyesha ajali zimesababishwa na ubovu wa magari na uzembe wa madereva, hatutaruhusu gari lisilokuwa na ubora kuendelea kubeba wanafunzi," alisema Mutafungwa.

Aidha, Kamanda Mutafungwa, alimuagiza Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Mwanza, Sunday Ibrahim kuhakikisha wakaguzi wa magari hayo wanakuwa na vifaa vinavyohusika ili kila gari likaguliwe kwa kuzingatia vigezo na maelekezo aliyotoa.

Kamanda Mutafungwa alisema kuwa ukaguzi wa magari ya shule zote zilizoko Wilaya ya Nyamagana na Ilemela utafanyika katika eneo la maegesho ya gereji iliyopo nyuma ya Stendi ya Nyamhongolo, wilayani Ilemela.

Alisema wilaya zingine zinatakiwa kupeleka magari yao katika vituo vya polisi katika wilaya husika kabla shule hazijafunguliwa.

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani mkoani hapa, Sunday Ibrahim, alisema tayari magari zaidi ya 50 yamefikishwa katika gereji hiyo kwa ajili ya ukaguzi ambao unafanyika bila malipo yoyote.

Aidha, alisema watatembelea shule zote kwa ajili ya kubaini watakaokaidi agizo hilo.

Akizungumza kwa niaba ya wamiliki wa shule, Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Wamiliki wa Shule Binafsi mkoani Mwanza, Ezekiel Molel, aliwataka wenye magari kupeleka magari yao kukaguliwa.

Mwenyekiti Baraza la Usalama Barabarani mkoani Mwanza, Ferdinand Chacha alisema: "Magari yatakaguliwa, wanatakiwa wamiliki kuajiri madereva walio makini, ukiwa na gari nzuri lakini dereva hayuko makini ni lazima ajali zitatokea tu. Hivyo nawaomba madereva tuongeze umakini ili kupunguza ama kuondoa ajali kwa watoto wetu"

Katika ukaguzi huo magari zaidi ya 50 yaliyofikishwa kituoni hapo, kufanyiwa ukaguzi kabla ya kuruhusiwa kuanza kutoa huduma pindi shule zitakapofunguliwa.



Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, akizungumza na wagonjwa waliokuwa katika foleni ya kuingia katika hema la Taasisi ya Jakaya Kikwete (JKCI), kwa ajili ya kupatiwa matibabu katika kliniki iliyoandaliwa ya matibabu bure kwa wananchi wa jiji hilo jana. **PICHA: BEATRICE SHAYO**

# RUWASA yahamasisha matumizi majisafi, salama

**Na Alex Sayi,** MASWA

WAKALA wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), wilayani Maswa mkoani Simiyu, wameitaka jamii kujenga tabia ya kutumia majisafi na salama ili kuepuka magonjwa ya mlipuko.

Hayo yamebainishwa na Mratibu wa Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOS), Wilson Magaigwa wakati wa mkutano na mwaka wa wadau wa sekta ya maji.

Magaigwa alisema kumekuwepo na mwamko mdogo wa utumiaji wa maji safi na salama kwa wakazi na wananchi wilayani hapa, hali inayosababisha miradi mingi kushindwa kujiendesha yenyewe.

"Ukiangalia wilaya yetu kila mwaka tunakabiliwa na mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu na hii inatokana na mwamko mdogo wa utumiaji wa maji safi na salama na badala yake wananchi wanatumia maji ya mito na mabwawa ambayo siyo salama" alisema Magaigwa.

Meneja wa RUWASA wilayani Maswa, Lucas Madaha, alisema kwa sasa wana hudumia vijiji 109 vyenye watu 356,566, wanao pata maji safi na salama ni 265,998 sawa na 74.6%, huku kukiwa na vituo vya kutolea maji 2,069 kati ya 2,155 vilivyopo, visima vifupi,1,552 na vituo vya miradi ya bomba 360.

Alisema Wilaya ya Maswa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 imetengewa Sh. bilioni 4.9 kupitia PforR-IV ili kutekeleza miradi ya maji, Ipililo, Kinamwigulu, Mwang'handa, Sayusayu na Ng'haya.

Alisema bajeti ya mwaka 2024/2025 imetengwa Sh. bil.3.7 kwa ajili ya kutekeleza miradi maeneo ya Budekwa, Kiloleli na Mwabayanda.

"Tunaishukuru serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji vijijini, kwa lengo la kumtua mama ndoo kichwani na ukiangalia katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Mei 2024 (RUWASA) imepokea zaidi ya Sh.bil.9.5." alisema Madaha.

Diwani wa Kata ya Ng'wingwa, Stiven Dwese alisema kuwa (RUWASA) inatakiwa kubainisha vigezo vinavyotumika kupeleka huduma ya maji kwa wananchi ili kuondoa dhana ya upendeleo wa utekelezaji wa miradi hiyo kwa majimbo yote mawili Maswa Mashariki na Magharibi.

Wakizungumzia hali ya kuchota maji ya kutumia kwenye madimbwi na chemchemu, baadhi ya wananchi wanaoishi kayika vijiji vya wilaya hiyo, walidai gharama za upatikanaji wa maji safi na salama ni kubwa jambo ambalo linasababisha kushindwa kumudu huduma hiyo.

"Yani maji safi na salama yapo lakini huku ni vijijini watu wengi hawana uwezo wa kununua maji hayo, inabidi warudi kutumia ya kwenye madimbwi, ndoo moja inauzwa Sh. 40 wengine hadi Sh. 70 hali hii inawashinda watu, tunaomba suala hili litafutiwe ufumbuzi angalau ndoo iuweze Sh. 20,"alisema Sagida Mitinje mkazi wa Kijiji cha Bushashi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Maswa, Paul Maige, alisema kuna haja (RUWASA) kutoa mgawanyo sawa kwenye utekelezaji wa miradi ya maji vijijini, ili kuondoa malalamiko na manung'uniko kutoka kwa baadhi ya madiwani na wananchi.

# Ukusanyaji kodi kwa mabavu kwamchefua RC

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha, amewaonya watumishi ambao wamekuwa wakikusanya mapato waache kutumia nguvu.

Alitoa onyo hilo juzi wakati akitoa salamu za viongozi wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu kilicholenga kujadili utekelezaji wa maagizo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Alisema ukusanyaji mapato ni nguzo ya halmashauri, kwamba itatekeleza shughuli zake kwa ufanisi, isije tumika nguvu kubwa wakati wa ukusanyaji wa mapato, bali wananchi wapewe elimu na kulipa kwa utaratibu.

"Tuzingatie ubinadamu wakati wa ukusanyaji mapato na siyo kutumia nguvu kubwa, elimu itolewe kwanza juu ya umuhimu wa kulipa mapato na wale ambao watakaidi fuateni taratibu ikiwamo kushirikisha polisi,"alisema Macha.


Aidha, aliwasisitiza wataalamu kubuni vyanzo vipya vya mapato, pamoja na madiwani kuhamasisha wananchi kulipa mapato kupitia kwenye mikutano yao, huku akiipongeza Halmashauri ya Kishapu kwa kupata hati safi kutokana na kujibu hoja za CAG na kutoa angalizo wasije wakalewa sifa bali waendelee kuchapa kazi kwa bidii na kufuata taratibu zote za utumishi.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, Emmanuel Johnson, alisema zamani halmashauri hiyo ilikuwa kwenye nafasi ya 10 bora ya halmashauri hapa nchini yenye hoja nyingi za CAG.



Ukurasa 12

**VIONJO VYA UTAFITI 2014...**
**TAKUKURU yaingia kazini na Uchaguzi wa Serikali Mitaa**



Ukurasa 14

**JAJI JACOBS MWAMBEGELE**
**INEC inazingatia mambo haya kuboresha daftari la wapigakura**



# Itungwe sheria mpya ya uchawi, kukomesha mauaji wenye ualbino

**NA GAUDENSIA MNGUMI**

MWAKA 2015, Rais Jakaya Kikwete, alihutubia taifa kupitia televisheni na kuapa kukomesha mauaji ya wenye ualbino aliyoeleza kuwa yameliletea taifa aibu na fedheha.

Alieleza kushtushwa na kuhuzunishwa na ongezeko la ghafla la mauaji haya makubwa lakini yanayoshangaza dunia. Cha ajabu, leo taifa linarudi tena kule gizani ambako miaka ya 2015, ilikuwa aibu kwa Tanzania.

Mauaji ya wanaoishi na ulbino ni aibu inayoeleza namna ambavyo tamaa ya madaraka mfano wanasaka vyeo, mali wanaochimba madini migodini na wale wanaoshiriki ushirikina wanavyosababisha watu washindwe kufikiri sawasawa, wakiamini kuwa fedha zinatoka kwenye miili ya watu.

Katika dunia iliyostaarabika ambayo maarifa ya kila aina yanayopatikana kiurahisi kwenye mitandao na madarasani ni aibu kuwa bado Watanzania wanawaua albino kwa lengo la kupata utajiri, madaraka, sifa na chochote kiwacho.

Leo hii ukitaka kujua namna bora ya uchimbaji madini, kuhutubia jukwaani, kufuga kisasa na kutengeneza mbolea au viuatilifu asilia unavipata kiganjani kwenye simu janja.

Haya ni maarifa ya kufanikisha ufaulu kwenye maisha lakini cha muhimu ni kutumia akili na kujiletea mafanikio, swali linabaki maarifa ya kuua albino watu wanayatoa wapi? Kwenye mtandao gani?

Tanzania ilichafuka kwenye vichwa vya habari duniani kwa matendo ya kuua wanaoishi na ualbino. Nchi yenye kiwango cha juu cha asilimia 85 watu wazima wanaojua kusoma, kuandika na kuhesabu kwa mujibu wa Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni, la Umoja wa Mataifa (UNESCO), inawezaje kuendeleza fikra za ushirikina hata wa kuua wanadamu?

Kiwango cha kujua kusoma, kuandika kinamaanisha uwezo kielimu si duni, wanaweza kuchambua mambo zaidi, sasa inakuwaje kuwaza kuwa viungo vya alibino vinatajirisha na kubadili maisha?

Ni wazi kuwa taifa limeumbuka kutokana na kuendekeza ushirikana na imani za kichawi kunakolisababishia taifa kuwa na imani kuwa viungo vyao vitawezesha kushinda nafasi za uongozi.

Wafanyabiashara kufanikiwa mara 100 kwenye shughuli zao na pia eti wanawake hasa wa familia za matajiri wasiozaa kupata mimba za watoto mapacha watatu, yote haya ni aibu.

Mwaka 2017 Umoja wa Mataifa, ulikadiria kuwa takriban watu 80 wenye ualbino nchini waliuawa tangu mwaka 2000, lakini takwimu hizo zinaweza kuwa kubwa zaidi kutokana na mashambulizi haya ya kikatili kufanywa kwa siri.

Mei 30, 2024 mtoto Asimwe Novath anadaiwa alichukuliwa na watu wasiojulikana nyumbani kwao Muleba huko Kagera, lakini licha ya kutafutwa hakupatikana akiwa hai hadi wiki iliyopita Juni 17 mwili wake ulipopatikana ukiwa ndani ya kiroba na baadhi ya viungo kunyofolewa.

Taifa limesikia na kushuhudia



Asimwe Novath

mauaji ya mtoto Asimwe Novath (2). Pengine sasa nikulikumbusha bunge kuwa ndiyo taasisi inayotegemewa na kuheshimiwa na wananchi kwa kuwa inabeba jukumu la uwakilishi, kuanzia maoni ya wapigakura, matumaini, kero zinazowaumiza, ndoto zao na matamanio mema na zaidi kuwapa majibu na ufumbuzi wa kila kitu kinachowaumiza.

Kwa hiyo, iisimamie serikali ifanyekazi kama mtumishi wa wananchi kulinda maisha ya Watanzania na wenye ualbino ambao ni sehemu raia milioni 61 wa taifa hili.

Wawakilishi wa wananchi wanapojadili mustakabali wa taifa ni lazima waje na majibu ya kupata Tanzania yenye maisha ya kimafanikio na furaha kwa watu wake wote ambao ndani yake wamo wenye ualbino.

Mijadala ya bajeti ya serikali 2024/25 iangalie namna ya kufanikisha kampeni za elimu na kuhamasisha jinsi ya kupambana na ushirikina na unyanyapaa wa watu wanaoishi na ualbino.

Kampeni za ulinzi wa wenye ualbino zifahamishe wahusika hasa mikoa na kanda zenye taarifa za mauaji kuwa ualbino si ugonjwa ni hitilafu kwenye jeni na kwamba si kitu cha kuhitaji tiba.

Serikali ifanikishe sensa ya kuwatambua na kuwapa huduma muhimu, elimu lakini pia kutibiwa macho ili kuondoa uoni hafifu. Wapate matunzo sahihi ya macho na kufuatilia ngozi zao kama zina matatizo.

Waelimishwe watu wa kutoa huduma kwa wenye ualbino kwenye vituo vya afya, wapate miwani, dawa na mafuta ya kuwakinga na jua. Wahudumu wawepo kwenye vituo vya msingi vya huduma kuanzia zahanati na vituo vya afya. Kila mara wataalamu wa macho na wa kuchunguza na kutunza ngozi wawasaidie.

Kama inajulikana kuwa wanaoishi na ualbino wanaweza kutekwa, kusafirishwa kutoka kijiji au mkoa mmoja hadi mwingine, kuuawa na kukatwa vipande vya miili yao, au makaburi ya kufukuliwa na kuondolewa viungo vyao, kwanini hilo lisikomeshwe?

Iwapo vifaru na tembo wanalindwa tena kwa gharama kubwa vipi kuhusu albino ambao ni wanadamu wanaostahili kulindwa na kuheshimiwa utu wao na zaidi kuhakikishiwa haki ya kuishi, kwa Watanzania hawa si zaidi?

Juhudi hizi ziwe endelevu ili Watanzania hawa waishi kwa amani na mauaji yao yatokomezwe na mara kwa mara wauaji, wanaowanyanyapaa wasipewe nafasi.

Ni vyema pia mamlaka mbalimbali hasa viongozi zinapoteuliwa wawepo na watu wanaoishi na ualbino ili kuongeza juhudi za kuwalinda na kuwatetea popote walipo.

VIONJO VYA UTAFITI WALIOFANYA 2014...

# TAKUKURU yaingia kazini na Uchaguzi wa Serikali Mitaa



Wapigakura katika maandalizi ya uchaguzi, wakisoma majina yao. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Renatha Msungu,**

**DODOMA**

WATANZANIA wanaelekea katika vipindi vya uchaguzi, ngazi serikali ya mtaa ni mwisho wa mwaka huu.

Ni msimu wenye ishara na minong'ono ya nguvu za rushwa. Kama ilivyo jina na wajibu wake wa msingi, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Dodoma, imeamua kuingia kazini.

Ni hatua inayoendana na wajibu wake wa msingi, kuzuia rushwa kabla ya kutokea na iwapo inatokea, inapambana nayo.

Kwa hatua ya mwanzo, taasisi hiyo Dodoma, imejipanga kuelimisha wananchi, namna ya kupata viongozi bora kupitia uchaguzi wa serikali mitaa.

Hapo, wananchi wanatakiwa 'kukaa mkao wa kula', kuhakikisha wanaelimika jinsi ya kukataa rushwa.

Kamanda wa TAKUKURU mkoani Dodoma, John Joseph, anataja mikakati waliyojiwekea ni kutoa elimu ya jamii, wakiwakumbusha adha ya kupokea na kutoa rushwa.

Joseph anaeleza, wako mbioni kuanza kampeni ya elimu kwa wananchi mkoani humo kuhusu vitendo vya rushwa na hasa kipindi kilichoko kuelekea Uchaguzi Serikali za Mitaa.

Mnamo Mei 10 mwaka huu, Kamanda Joseph, aliendesha darasa kwa wanahabari kuhusu rushwa kuelekea kipindi cha Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

"Sasa baada ya kuwapatia semina ninyi waandishi tunaenda kwa wananchi na tutatoa semina kwa njia ya mikutano ya hadhara na tutapita maofisini kutoa semina.Pia, kadri ya muda utakavyoruhusu hivyo tunatarajia kupata ushirikiano mkubwa sana kutoka kwa wananchi," anasema.

Anasema kanuni za uchaguzi ujao wa wenyeviti wa vijiji, wajumbe wa halmashauri za vijiji na wenyeviti wa vitongoji katika mamlaka za wilaya ya Mwaka 2019, imetoa utaratibu wa uchaguzi usiokuwa na rushwa.

Kamanda Joseph anasema, wanawaelimisha wananchi namna ya kuikabili rushwa kuelekea uchaguzi huo wa mitaa, ikiwamo suala la jamii kurubuniwa kupewa rushwa wawachague viongozi wanaowahonga.

Hilo analifafanua, wamelenga kuhakikisha uchaguzi ujao unatoa viongozi bora wasiopatikana kwa njia ya fedha, ili waweze kupita katika uchaguzi za serikali za mitaa.

Anafafanua kuna jamii zimekuwa zikikubali kurubuniwa, kitendo kisichokubalika, kutokana na taifa kuhitaji kupata viongozi bora na 'si bora kiongozi'.

**WANANCHI NA YAO**

Wananchi wanataja suala la rushwa ni changamoto, wakiiomba TAKUKURU ifanye kazi kuelimisha jamii kuhusu kutopokea rushwa wakati wa uchaguzi wa serikali za mitaa.

Gloria Lyimo, anashauri ikifanyika hivyo, itakuwa imewasaidia sana kupata 'viongozi bora' na si 'bora viongozi' watakaosaidia usimamizi wa maendeleo.

Anafafanua, suala la rushwa limebaki kuwa changamoto ya jamii, hivyo wananchi wanapaswa kuwa mstari wa mbele kusikiliza elimu yake.

Joseph anafafanua kwamba wananchi wanahitaji elimu ya kupinga na kutopokea rushwa, wakati wa uchaguzi wa serikali unaokuja.

Mkazi Hamis Juma, anasimulia kwamba jamii imekuwa ikirubuniwa na vitu vidogo vya rushwa na kushindwa kuchagua viongozi bora, akinena:

"Tunaishukuru TAKUKURU imekumbuka mapema kuanza kutoa elimu hivyo itasaidia watu kuwa makini na suala la rushwa."

Anaishauri TAKUKURU kabla ya kuandaa mikutano hiyo, inapaswa kuandaa mikutano ya hadhara itakayosaidia kuelimisha watu kuhusu rushwa.

Pia, anaitetea taasisi hiyo haijachelewa muda wa elimu kwa umma, ili kujua kiwango cha uelewa kuhusiana na rushwa.

Mkuu huyo wa TAKUKURU, anasema wamepanga kutoa elimu katika mkoa wote juu ya kukataa rushwa katika uchaguzi na mapana yake.

> TAKUKURU ilifanya utafiti mwaka 2014, ikinuia kuzishauri mamlaka zinazohusika, njia bora za kudhibiti rushwa katika uchaguzi nchini. Ni utafiti uliogusa maeneo ya: Kubaini mianya ya rushwa katika mchakato wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2014; Kutathmini uelewa wa wananchi kuhusu haki na wajibu wao kwa uchaguzi huo.

**UTAFITI MITAA 2014**

TAKUKURU ilifanya utafiti mwaka 2014, ikinuia kuzishauri mamlaka zinazohusika, njia bora za kudhibiti rushwa katika uchaguzi nchini. Ni utafiti uliogusa maeneo ya: Kubaini mianya ya rushwa katika mchakato wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2014; Kutathmini uelewa wa wananchi kuhusu haki na wajibu wao kwa uchaguzi huo.

Maeneo mengine yakatajwa ni kuainisha vitendo vya rushwa vilivyojitokeza katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2014; na kushauri namna ya kuziba mianya yake katika uchaguzi unaofuata.

Ni utafiti uliofanyika katika mikoa ya Tanzania Bara na wakahojiwa watu 1332, katika mgawanyo wa kila wilaya na kata zake mbili zilizochaguliwa; huku ndani ya kata hizo, zilizochaguliwa kuna ama mitaa au vijiji viwili.

Makundi ya wadau waliohojiwa ni: wananchi, wagombea na wasimamizi wa uchaguzi. Aidha, taarifa za msingi za utafiti huu zilikusanywa kwa njia ya mahojiano na usaili na kwa kuangalia matukio, ambapo madodoso na orodha ya ukaguzi zilitumika.

Taarifa za upili zilikusanywa kwa kupitia nyaraka zilizohusu uchaguzi, matokeo ya utafiti kabla, wakati na baada ya uchaguzi ni kama ifuatavyo:

Kabla ya uchaguzi, baadhi ya wasimamizi wa uchaguzi hawakutoa orodha ya majina ya wapiga kura, hawakuonyesha mipaka ya mitaa, vijiji na vitongoji.

Vilevile, baadhi ya wapigakura hawakutaka kujiandikisha kwenye daftari la wapigakura, baadhi ya wagombea kutoidhinishwa na vyama vyao vya siasa, kukosekana barua za wadhamini na nyaraka pingamizi za wagombea ambao hawajaridhika na uendeshaji uchaguzi.

Sababu za pingamizi hizo zikatajwa ni kwa baadhi ya wagombea kutowekwa wazi; kampeni kufanyika zaidi ya muda unaokubaliwa kisheria; chama kimoja kuingilia kampeni ya kingine.

Mengime ni kuwapo uelewa mdogo wa wapigakura kuhusu sheria, kanuni na taratibu za uchaguzi pamoja na matumizi ya lugha za matusi, kashfa na kejeli.

Aidha, utafiti unaonyesha, baadhi ya wapiga kura walisafirishwa toka eneo moja kwenda lingine kinyume na taratibu; majina ya baadhi ya wagombea kutoonekana vituoni; kutokuwapo faragha ya kupigia kura; na upungufu wa vifaa vikiwamo karatasi za kura.

Ripoti pia inataja; kuendelea kampeni hata wakati wa kupiga kura; kutokufunguliwa kwa wakati vituo vya kupiga kura; picha za baadhi ya wagombea kuchanwa; na kukosekana wakala wa baadhi ya vyama vya siasa.

Utafiti huo unataja kuwapo vitendo vya rushwa katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kama ujao, ikihusu ugawaji fedha taslimu, khanga, mashati, kofia, vinywaji na vyakula, mifuko ya saruji, sare za michezo, ili kuwashawishi wapiga kura.

Katika baadhi ya vituo kunatajwa kulichelewa kuhesabiwa kura, hata kusababisha vurugu na fujo; na vitendo vya dalili za rushwa, vyote vukichangia kurudiwa uchaguzi katika baadhi ya maeneo nchini.

**MAPENDEKEZO UTAFITI**

Kutokana na matokeo ya utafiti huo, kuna mambo kadhaa yamependekezwa kuziba mianya ya rushwa kwa uchaguzi nchini.

Hapo kunatajwa suala la elimu kuhusu haki na wajibu wa mpiga kura katika mchakato wa uchaguzi, kama inavyofanyika sasa mkoani Dodoma.

Pia, kunatajwa suala la kuimarisha vyombo vinavyohusika na usimamizi sheria, pia taratibu za uchaguzi; vyama vyote vya siasa vinavyoshiriki katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa, na Uchaguzi Mkuu vinapaswa kuzingatia maadili wanayokuwa waliyoyaridhia pamoja kukuza demokrasia nchini.

Pia, kuna suala la wasimamizi uchaguzi wanapaswa kutekeleza wajibu wao kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za uchaguzi; na kujiepusha na itikadi za kisiasa au vitendo vinavyoashiria upendeleo, rushwa au ushabiki wa kisiasa.

# Rais Ruto anapokubali kukutana na vijana wanaozigomea kodi



Waandamanaji mjini Kisumu Jumatano iliyopita. **PICHA: VOA**

**Na Ani Jozeni**

RAIS William Ruto, anafanya juhudi za kumaliza mzozo wa kukataa hatua za ongezeko la kodi zilizofanywa katika mapendekezo ya bajeti ambayo yameshapitishwa.

Kinyume na matarajio, Ruto anasimama jukwaani kuwasifu vijana kwa kutoka mbele na kuweka wazi madai yao, kwa njia ambayo haikwepeki kwa jamii na viongozi walioko madarakani kupata ujumbe.

Hata hivyo haikuwa rahisi kusema nini kinafuata baadaye, kwani bajeti ilishapita na sheria ya fedha iko mbioni.

Moja ya maeneo tata ya suala hilo ni uwezo wa Rais Ruto kuongea na vijana wakati suala hilo liko bungeni na tayari kura ilishapita, hivyo kuhitaji ifumuliwe upya ili maongezeko hayo yaondolewe. Ndicho wanachotaka vijana na kama ilivyo kawaida katika masuala ya maandamano, hakuna hoja za jinsi ya kujazia pengo hilo, ila tu kutaka iwepo amani kwa kuondoa nyongeza za kodi maisha yasiwe magumu zaidi.

Endapo Rais Ruto yuko tayari kuzingatia hoja hizo, itabidi pia apate majawabu nini kinaweza kufanyika, nje ya kodi hizo.

Suala la awali ni kama mwelekeo huo unaweza kudumu, kuwa yafanyike majadiliano kati ya serikali na vijana, au huo ni mwanzo tu wa kuanza kuvuruga wimbi hilo. Zipo njia kadhaa za kumaliza mawimbi ya madai kuhusu kile serikali inachofanya, na hatua ya maandamano ya vijana ni tishio la awali kuhusu mwelekeo wa serikali.

Ikifikia hatua ya kuitisha migomo ya wafanyakazi, unaweza kusema hali sasa inaanza kuwa mbaya, kwani haifikii uasi wa taasisi za nchi kirahisi.

Uasi ndiyo kielelezo kuwa serikali hiyo haitakiwi, na endapo ni suala la kura ni kuwa hali hiyo haifikiwi katika mazingira ya kidemokrasia.

Mfumo wa kidemokrasia hauna uasi wa taasisi za nchi kwani mifumo ya utii inabaki ilivyo, watu wakivumilia hao walioko madarakani wamalize muda wao. Halafu jamii inajipanga upya nchi ipate mwelekeo mwingine, iwe ni chama kingine kuingia madarakani au serikali ibadilishwe kwa kina, kulingana na mazingira.

Kabla rais hajaanza mazungumzo ya aina yoyote tayari atakuwa amepima ushauri wa aina tofauti, akijua kuwa kila kitu mwishowe kinaishia bungeni.

Anaweza kuchukua hatua za hapa na pale na kutazamia kuwa zitatimia bungeni, ila siyo wazi kama atarudia pendekezo lake la kubinafsisha mashirika ya umma ambayo ni mzigo serikalini, kugeuza madeni yake yawe hisa za uwekezaji ili kupunguza kiwango cha kulipia madeni katika bajeti ya nchi ambacho kiko juu mno.

Baadhi ya vijana walipitisha mabango yenye matusi ya nguoni, hata mtu unaogopa kama baadhi watakuwa salama kama serikali itaamua washughulikiwe.

> Moja ya tafsiri ni kuwa 'watazikwa' katika uchaguzi mkuu ujao, jambo ambalo linaleta hoja kinzani kama kura za vijana mwaka 2027 zitakuwa ni sehemu gani ya kura zote.

Tayari kuna taarifa kuwa baadhi ya waandamanaji wamedakwa huko maskani yao, ila bado ni mapema kujua kama wanafunguliwa mashtaka au hapana, ila kunachohofiwa ni kama itokee kuwa wanapotea.

Siyo jambo la ajabu katika siasa za upinzani au kuhakikisha umoja wa nchi pale wanapotokea watu wanaonyesha dharau kwa mamlaka iliyopo, na si jambo la kushangaza ni kuwa hayaishi kutokea katika mazingira tofauti.

Ina maana kuwa haya maandamano yanaweza kuwa hatua nyingine ya wananchi, na hasa hao vijana kuelewa mipaka ya demokrasia na kujizatiti kuiheshimu zaidi.

Bado hakuna uhakika, au ishara, kama Rais Ruto atarudisha mpango wake wa ubinafsishaji kama njia ya kutokea katika maandamano, kwani muswada huo ulishapita bungeni, na hitaji la kubinafsisha halikuleta mzozo.

Kimsingi tabaka la watawala nchini humo hawako tayari kujadili ubinafsisha ila hawana tatizo na ongezeko la kodi, wakati vijana hawakutajwa wakati wa mzozo kuhusu ubinafsishaji, wakiwa pembeni na kungojea wazee watatue masuala hayo, ila hili la kodi wakaamua kulivalia nguja kwa uhamasishaji katika mitandao ya kijamii.

Bado hakuna uhakika wimbi hilo ni la kina kiasi gani na ni kwa kiwango gani linaweza kufikia mahali bunge lihitajike kuamua.

Labda mtu unaweza kuangalia kibwagizo cha maandamano hayo na baadhi ya ishara zake, kwa mfano kubeba majeneza barabarani eti ya wabunge waliounga mkono hoja ya kuongeza kodi, ambako baadhi ya wachambuzi wa habari walijaribu kufafanua, au kupata picha ya dhamira yake halisi.

Moja ya tafsiri ni kuwa 'watazikwa' katika uchaguzi mkuu ujao, jambo ambalo linaleta hoja kinzani kama kura za vijana mwaka 2027 zitakuwa ni sehemu gani ya kura zote.

Serikali ina kazi ya kufurahisha wizara na idara tofauti za serikali, halafu tawala za majimbo kuhusu mpangilio wa raslimali pamoja na kodi kwa mwaka ujao, na kama hayo yalishakubaliwa, vijana watatoa hoja zipi kuyapangua?

Kinachoweza kufanyika labda kuandaa mpango wa kuwasaidia vijana hapa na pale, iwe ni mfuko wa kusaidia miradi yao, kupunguza kodi kwa wajasiriamali wa ngazi hii au ile, na masuala kama hayo.

Maandamano ya vijana nje ya madai halisi ya kidemokrasia kama Senegal na kwa uchache zaidi Uganda siyo rahisi kufikia malengo yake, yanapoanza kuingilia kazi za bunge, kutunga sheria na kupitisha bajeti, hata kuanza kumtukana rais wa nchi.

JUKWAA LA VIONGOZI

## JAJI JACOBS MWAMBEGELE;

# INEC inazingatia mambo haya kuboresha daftari la wapigakura



Mwenyekiti wa INEC, Jaji Jacobs Mwambegele, wakati akitoa taarifa za masuala ya uchaguzi. **PICHA: NEC**

**Na Sabato Kasika**

KUPIGA kura ni jukumu lako. Linakuhusu, hayo ni maoni ya muhimu, kutoka wadau wanaochagiza demokrasia na uhuru wa kuchagua viongozi.

Mdau mkuu ni Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), hasa inapohamasisha taifa wakati huu linapoelekea kwenye uchaguzi mkuu wa kumpata rais, wabunge na madiwani unaotarajiwa mwishoni mwa mwaka 2025.

Ili kufanikisha uchaguzi kazi ya kuboresha daftari la kudumu la wapigakura, inatarajiwa kuanza Julai 20, 20024 na kabla ya kazi hiyo, ni vyema kuwaamsha wenye nia ya kupigakura kuwa huu ndiyo wakati wa kuboresha taarifa zao.

Hapa sio kuwa na sifa za kujiandikisha au kuboresha taarifa tu, bali pia ni vyema kuwatambua wale ambao hawatakuwa na sifa za kujiandikisha ama kuboresha taarifa zao katika daftari hilo.

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inataja baadhi ya vifungu vya sheria ya uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani ya mwaka 2024 vinavyoelezea sifa za kupigakura au kukosa vigezo vya kushiriki kwenye jukumu hilo.

Mwenyekiti wa INEC, Jaji Jacobs Mwambegele, anasema, uboreshaji huo unazingatia sheria hiyo pamoja na kanuni za uboreshaji wa daftari hilo za mwaka 2024.

"Sheria inaelezea kwa kina mtu mwenye sifa za kuandikishwa kuwa mpigakura na yule ambaye hana sifa za kuandikishwa kuwa mpigakura, hizo zote ni muhimu wananchi wazijue," anasema Jaji Mwambegele.

Anakariri baadhi ya vifungu vya sheria hivyo vinayoelezea kuwa sifa za kujiandikisha kuwa mpigakura au kukosa sifa za kushiriki kuchagua viongozi kuwa ni ibara ya 9,- (1).

"Katika ibara ya 9,- (1), inasema, mtu yeyote ambaye ni raia wa Tanzania aliyetimiza umri wa miaka 18 na ambaye hajapoteza sifa chini ya sheria hiyo au sheria nyingine yoyote, atastahili kuandikishwa kuwa mpigakura chini ya masharti ya sheria hiyo," anasema.

Anaongeza kuwa kifungu cha (2) cha sheria hiyo kinaelezea kuwa, bila kujali masharti ya kifungu cha (1), na kwa kuzingatia uthibitisho wa umri, Mtanzania yeyote ambaye hajapoteza sifa chini sheria hiyo au sheria nyingine yoyote ambayo wakati au kabla ya tarehe ya uchaguzi atakuwa ametimiza umri wa miaka 18, atastahili kuandikishwa kuwa mpigakura.

"Lakini ibara ya 10,- (1) inataja mtu asiye na sifa za kujiandikisha kuwa mpigakura ni pamoja na kuwa raia wa nchi nyingine tofauti na Tanzania," anasema.

Anaongeza mwingine ni yule ambaye imethibitika kuwa hana akili timamu au amewekwa kizuizini kama mhalifu, au amewekwa kizuizini kwa ridhaa ya Rais, ametiwa hatiani kwa kosa ambalo adhabu yake ni kifo," anasema.

Anafafanua kuwa eneo hilo la sheria linagusia pia anayetumikia kifungo kwa kosa ambalo adhabu yake inazidi miezi sita iliyotolewa na mahakama au kama ilivyobadilishwa na mamlaka nyingine.

"Vilevile, mtu atakuwa amepoteza sifa za kuandikishwa kuwa mpigakura chini ya masharti ya sheria hii au nyingine yoyote inayotumika kuhusu makosa yanayohusiana na uchaguzi wowote," anasema.

**MAELEKEZO ZAIDI**

Kabla ya kuanza kuboresha, anasema INEC inatoa maelekezo muhimu ya kuzingatiwa, ambayo ni mwananchi kufika katika kituo cha kuandikisha wapigakura kuonana na waandishi au makarani wanaohusika kueleza dhamira ya kutaka kuandikishwa kupigakura au kuboresha taarifa zake.

Iwapo karani msaidizi atarídhika kuwa anayetaka kuandikishwa ana sifa, atajaza fomu inayohusika na eneo hilo wakati anayeboresha taarifa, atajaza fomu nyingine kuboresha au kuhamisha taarifa. Wakati huo huo pia kuna fomu nyingine inayojazwa, kama mwananchi anataka kufuta taarifa za mpigakura aliyekosa au kupoteza sifa.

Vilevile, atatakiwa kuonana na wataalamu wa vifaa vya bayometriki vinavyoandaa taarifa za mpigakura kwa kuchukua alama za vidole, saini na picha na kuziingiza katika mfumo wa kielektroniki kulingana na ombi alilowasilisha, kisha atapatiwa kadi.

"Lakini mpigakura anaweza kuanzisha mchakato wa awali kwa njia ya mtandao ili kuboresha taarifa zake au kubadilisha taarifa zake, kuhamisha taarifa kutoka kituo cha awali kwenda kingine kwa kufuata maelekezo ya tume," anasema.

Anawaelekeza kuingia katika tovuti ya INEC ambayo ni ww.inec.go.tz kwa kutumia kompyuta au simu janja na kubonyeza kiunganishi kilichoandikwa boresha taarifa za mpigakura.

"Vilevile, mpigakura anaweza kutumia anuani ya ovr.inec.go.tz ambayo itampeleka moja kwa moja kuanzisha mchakato ambapo mfumo utamletea ukurasa wenye vipengele vitatu," anasema.

Anasema, mfumo utamjulisha mpigakura papo hapo kuwa ombi lake limepokelewa, kisha ombi litafanyiwa kazi na tume, mpigakura atapokea ujumbe mfupi wenye kumbukumbu namba kupitia namba yake ya simu aliyotumia wakati wa kuboresha taarifa zake.

"Namba hiyo ya kumbukumbu atakwenda nayo kwenye kituo cha kuandikisha wapigakura kwa ajili ya kumalizia hatua zilizobaki na kupatia kadi yake ya mpigakura." Anaongeza Jaji Mwambegele.

**YA KUEPUKA**

Tume inaeleza kuwa yapo mambo ambayo ni muhimu mpigakura kuyaepuka wakati wa uboreshaji wa daftari hilo, ikiwamo kutoa taarifa za uongo kuhusu taarifa zake, mtu mwingine, kwa lengo la kuandikishwa kuwa mpigakura.

"Wananchi pia wanatakiwa kuepuka kuomba kuandikishwa zaidi ya mara au kutoa tamko la uongo kuhusu kupotea au kuharibika kwa kadi ya mpigakura ama kifo," anasema.

Mwenyekiti anaongeza kuwa ni muhimu kuepuka kununua au kuuza kadi ya mpigakura na kuiba au kuharibu kadi ya mpigakura, huku akisisitiza kuwa kujiandikisha kuwa mpigakura ni msingi wa uchaguzi bora.

Pamoja na hayo, Jaji Mwambegele anasema, katika kazi hiyo, tume inatarajia kuandikisha wapigakura wapya 5,586,433 nchi nzima, huku ikiboresha taarifa za wapigakura 4,369,531.

Aidha, anasema, wakati wa uboreshaji wa daftari, kuna makundi ambayo yatapewa kipeumbele katika foleni, wakiwamo wenye ulemavu, wajawazito, wagonjwa, wazee na kinamama wenye watoto wachanga.



## HABARI DODOMA

# SUA, Wizara ya Maji kutekeleza mradi ustahimilivu wa mabadiliko tabianchi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHUO Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kushirikiana na Wizara ya Maji kimeanza kutekeleza mradi wa ustahimilivu wa mabadiliko tabianchi katika nyanja za kitropiki, ili kupata suluhu ya shida ya maji katika maeneo yanayopata mvua chini ya kiwango.

Mradi huo utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu katika maeneo yenye shida ya maji ukiwa na lengo la kuangalia namna ya kukabiliana na mabadiliko tabianchi katika maeneo yanayopata mvua chini wastani kwa mwaka.

Mkurugenzi wa Uzamili, Utafiti, Uhaulishaji wa Teknolojia na Ushauri wa Kitaalamu (SUA), Prof. Japhet Kashaigili, alibainisha hayo juzi jijini hapo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa mradi huo katika Mkoa wa Dodoma.

Alisema mradi huo unalenga kuangalia namna bora ambavyo itasaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika maeneo ya kitropiki yenye shida ya maji juu ya ardhi.

“Mradi huu utatelezwa hapa Dodoma ikiwa ni moja ya eneo ambalo linachangamoto ya upatikanaji wa maji kwani Dodoma pia ni mkoa ambao unategemea chanzo cha maji Mzakwe chini ya ardhi katika Bonde la Makutupora,” alisema.

Alisema kutokana na mahitaji ya maji kuongezeka ipo haja ya kufanya utafiti wa mwenendo wa upatikanaji maji chini ya ardhi katika maeneo hayo ya kitropiki ambayo yanapata mvua chini ya milimita 500 kwa mwaka.

“Dodoma inategemea maji chini ya ardhi kupitia chanzo cha Mzakwe kilichopo Bonde la Makutupora kwa asilimia 60 hivyo lipo hitaji la kujua mwenendo wa maji katika chanzo hicho,” alisema.

Alisema kutokana na ongezeko la mahitaji ya maji katika Mkoa wa Dodoma ikiwamo shughuli za kibinadamu wao kama wataalamu wanapaswa kujua mwenendo wa maji chini ya ardhi na mahitaji yaliyopo ili kuweka mipango ya baadaye.

Aidha, alisema mradi huo ambao ulizinduliwa mwaka jana unatekelezwa kupitia maabara za mabadiliko.

Alisema kutoka na mipango inayofanywa na serikali kupitia Wizara ya Maji wao kama wataalamu wa vyuo vikuu wameona ipo haja ya kushiriki kutatua changamoto ya upatikanaji wa maji kwenye maeneo ya kitropiki.

“Hivi sasa kuna visima vingi vinachimbwa kwenye nyumba binafsi, hoteli hivyo ni muhimu sana kufahamu mwenendo wa maji chini ya ardhi na uhusiano wa ongezeko la matumizi ili baadaye tuweze kuja na mipango mizuri tusije tukashangaa kikatokea kitu kingine ambacho tulikuwa bado hatujajiandaa,” alisema.

Alisema katika utafiti huo wanahitaji kuujua mfumo mzima wa maji na shughuli za kibinadamu zinazoendelea.

“Tukiweza kufanya hivyo inamaana tunaweza kuona kitu gani kifanyike kuweza kusaidia uzalishaji wa maji kwenye maeneo mbalimbali lakini pia kuwa na angalizo twende mpaka hatua gani isije ikawa ni changamoto,” alisema.

Alisema utafiti huo wa miaka mitatu pia unalenga kuangalia namna ya kuleta suluhu mbalimbali katika suala hilo na wanafanya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Naibu Makamu wa Mkuu wa Chuo, Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaaluma SUA, Prof. Maulid Mwatawala, alisema Mkoa wa Dodoma ni sehemu ya nyanda kavu yenye shida ya upatikanaji maji, hivyo ipo haja ya kuangalia maji yaliyo chini na kuyatunza.

“Kwahiyo kundi hilo limekaa hapa kuangalia nini utakua mchango wa maji ambayo yapo ardhini katika kutatua changamoto za upatikanaji wa maji hapa Dodoma,” alisema.

Alisema athari za mabadiliko ya tabianchi ni nyingi ikiwamo maji kupungua na kutokuwapo kabisa.

## TIRA yakaa mguu sawa kupeleka elimu ya bima

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) imesema imejipanga kuwafikia Watanzania wengi katika mikoa mbalimbali ili kuwaelimisha kuhusu masuala ya bima.

Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu – TIRA, Hawa Mniga, alisema wamejipanga kuhakikisha wanapita katika mikoa na maeneo mbalimbali kuhakikisha wananchi wanajua umuhimu wa bima lakini pia wanapata elimu.

Alisema, TIRA imeendelea kutekeleza majukumu yake ikilenga kuwafikia Watanzania wengi kwa kuwaelimisha na kuwahamasisha kuhusu masuala ya bima.

Alisema mbali na hilo pia walitoa elimu kuhusu umuhimu wa bima, ushauri wa kitaalamu na fursa ya kuwasilisha malalamiko yao kuhusu huduma za bima wanazopokea.

Ushiriki wa TIRA katika maadhimisho haya ya Wiki ya Utumishi wa Umma umekuwa wa manufaa makubwa na TIRA itaendelea kuhakikisha soko la bima nchini linabaki salama na lenye manufaa kwa watumiaji wote wa huduma za bima kwa kuendelea kutumia majukwaa mbalimbali kutoa elimu kuhusu bima.

Hata hivyo, aliwataka wananchi kutokuwa wavivu wa kujifunza kuhusu bima, hivyo wanapopata wasaa wa elimu wanapaswa kuizingatia ili iwape manufaa hapo baadae.

Katika wiki ya utumishi wa umma iliomalizika hivi karibuni jijini Dodoma TIRA ilitoa elimu kwa watu waliohudhuria katika banda lao la maonyesho ya utumishi kwenye wiki hiyo.



Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omari Kipanga (kushoto), akizungumza na wanafunzi na walimu wa Shule ya Msingi St. Joseph ya Wilaya ya Mafia, mkoani Pwani, waliofika bungeni jijini Dodoma jana kwa ajili ya kujifunza shughuli za Bunge. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Dawa za mil.112/- zilizoisha muda kuteketezwa

**Na Thobias Mwanakatwe,**

MANYONI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Manyoni mkoani Singida inatarajia kuteketeza dawa zenye thamani ya Sh. milioni 112.8, kutokana na muda wake wa matumizi kupita.

Hayo yamebainika wakati wa kikao maalum cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya hiyo kilicholenga kujadili taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) katika mwaka wa fedha wa 2022/2023.

Mweka Hazina wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, George Mzeru, alisema katika taarifa ya CAG miongoni mwa hoja zilizoibuliwa ni dawa zilizoisha muda wake wa matumizi ambazo hazijateketezwa zenye thamani ya Sh.112, 831,973 ambazo zilikusanywa stoo kwa nyakati tofauti kuanzia mwaka 2019 hadi 2023.

Mzeru alisema mapendekezo ya mkaguzi ni kwamba menejimenti ipate vibali vya kuziteketeza dawa hizo ambapo zoezi la kuhakiki dawa zilizoisha muda wake lilifanyika Mei 25, 2024 na taarifa imewasilishwa kwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha ili kuziteketeza.

Kufuatia hali hiyo, Diwani wa Viti Maalum Blandina Mika alihoji inakuweje baadhi ya zahanati zinaupungufu wa dawa na wananchi wanateseka lakini zinateketezwa dawa za mamilioni ya fedha.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, alisema tatizo la kuacha dawa hadi zinakwisha muda wa matumizi yake lisijitokeze tena katika mkoa huu na kuagiza kuanzia sasa dawa ziwe zinaagizwa kulingana na mahitaji ya kila zahanati na hospitali.

“Juzi nilikutana na ‘case’ kama hii Halmashauri ya Itigi ambako nako kuna dawa za zaidi ya Sh.milioni 23 zinatakiwa ziteketezwe kwa kuwa muda wake wa matumizi umepita, niwaombe jambo hili Singida hatulitaki hata likitokea litokee dogo la kibinadamu lakini si kwa kiwango hiki,” alisema.

Dengedo alisema ni jambo la kushangaza Wilaya ya Manyoni kuja na hoja ya CAG ya ukosefu wa vifaa tiba vya Sh.milioni 60 lakini wakati huo kuna dawa za Sh.milioni 112 zinatakiwa kuchomwa moto kwasababu muda wake wa matumizi umekwisha jambo ambalo siyo sawa.

Naye Mganga Mkuu wa Wilaya Manyoni, Dk.Furaha Mwakafwila, alisema kwa muda wa miaka 10 wilaya hiyo haijawahi kutekeleza dawa lakini baadhi zilikuwa zinakuja wakati muda wake wa matumizi umekwisha.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, Jumanne Mlagaza, alisema kibali kikishatolewa dawa ziteketezwe kisisubiri kipite muda wake.





# Hekta 29,000 zaokolewa Nyanda za Juu Kusini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HEKTA 29,000 za misitu iliyokuwa hatarini kutoweka kutokana na shughuli za kibinadamu kwenye mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, zimeokolewa na serikali.

Hatua hiyo imefanikiwa baada ya kuwaondoa wananchi waliokuwa wanafanya shughuli hizo na kuwasaidia kuanzishia shughuli mbadala za kujiingizia kipato.

Shughuli zilizokuwa zinachangia kuharibika kwa misitu hiyo ni pamoja na ukataji wa miti kwa ajili ya kuni, uchomaji wa mkaa, ufugaji na kilimo kisichokuwa endelevu hasa kulima maeneo makubwa kwa kutumia teknolojia duni.

Mratibu wa Utekelezaji wa Mradi wa Urejeshwaji Endelevu wa Mazingira na Hifadhi ya Bioanuai kutoka katika Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, Dk. Damas Mapunda, aliyasema hayo jana jijini Mbeya kwenye kikao kazi cha watekelezaji wa mradi huo kutoka katika halmashauri saba za mikoa hiyo.

Alizitaja halmashauri ambazo maeneo ya misitu hiyo imeokolewa kuwa ni Halmashauri ya Iringa, Wanging'ombe mkoani Njombe, Mbarali na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kwa Mkoa wa Mbeya, Halmashauri ya Sumbawanga mkoani Rukwa na Mpimbwe na Tanganyika mkoani Katavi.

Alisema wananchi waliokuwa wanafanya shughuli zilizokuwa zinachangia uharibifu wa misitu hiyo wamesaidiwa kuanzisha shughuli endelevu ikiwamo kilimo kinachozingatia uendelevu wa mazingira, ufugaji wa ng'ombe wa kisasa, kilimo cha malisho na na ufugaji wa nyuki.

Alisema mradi huo unafadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa Mazingira kwa Dola za Marekani milioni 11.2 ambayo ni sawa na Sh. bilioni 27 na kwamba watekelezaji ni halmashauri na sekretarieti za mikoa inayohusika na mradi huo.

Baadhi ya watekelezaji wa mradi huo, walisema mradi huo umesaidia kubadili maisha ya wananchi ambao walikuwa wanategemea uchumi wao kwenye uharibifu wa misitu.

Ofisa kiungo wa mradi huo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Raphael Shitindi, alisema kupitia mradi huo wamechimba kisima kirefu katika Kijiji cha Matebete na kujenga birika la kunyweshea mifugo ili kupunguza uvamizi wa vyanzo vya maji.

Vilevile alisema wameanzisha kituo cha kuchakata maziwa katika kijiji hicho kwa ajili ya kuwasaidia kinamama ambao walikuwa wanauza kuni ili kuwasaidia kuachana na shughuli yao ya asili ambayo ilikuwa inaharibu misitu.

Pia alisema kupitia mradi huo wameanza kujenga majiko banifu kwenye taasisi mbalimbali za umma zikiwamo shule na magereza ili kupunguza matumizi ya kuni ambazo zinachangia kuharibu misitu.

Akifungua kikao hicho, Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Christina Mndeme, alisema asilimia 61 ya ardhi yote nchini iko hatarini kuharibika kutokana na shughuli za kibinadamu zisizokuwa endelevu.

Hivyo, aliwataka watekelezaji wa mradi huo kuhakikisha wanasimamia vizuri mradi huo ili uendelee kuleta matokeo ambayo yanakusudiwa na serikali ikiwamo kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.



Mkuu wa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, Kanali Denis Mwila (katikati mwenye kofia), akisaidiana na Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi, Godwel Ole Meing'ataki na mwakilishi wa Shirika la Six Rivers Afrika, Sam Ratcliffe, kukata utepe kuzindua uwanja mpya wa ndege uliojengwa ndani ya hifadhi hiyo, katika kijiji cha Ikoga, wilayani humo mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Watu wenye ulemavu waomba mil.13/- kufuga samaki

**Na Elizabeth John,**

WANGING'OMBE

SERIKALI wilayani Wanging'ombe mkoani Njombe, imeombwa kusaidia kikundi cha Manange cha watu wenye ulemavu wa viungo na uoni hafifu Sh. milioni 13, ili kufanikisha kuchimba mabwawa ya samaki sita na kupata vifaranga kwa lengo la kujikwamua na umaskini.

Ombi hilo limetolewa na wanakikundi hao katika Kijiji cha Itambo wilayani humo wakati wakizungumza na waandishi wa habari.

Walisema wanaiomba serikali kuwasaidia kupata mkopo ili kujenga mabwawa sita ambayo wanaamini yatawasaidia katika kujikwamua kiuchumi.

"Tungefanikiwa kupata haya mabwawa sita tutashukuru sana serikali yetu, hata wakitupa mkopo sisi tutarejesha vizuri na hitaji letu ni Sh. milioni 13," alisema Grayson Mkongwa.

Naye Stanely Mkongwa alisema tatizo kubwa ni kwamba wao hawana fedha ya kuwezesha kupata mabwawa na vifaranga vya samaki ili kuvipanda na baadaye wapate kipato kikubwa.

Aidha, alitoa rai kwa watu wenye ulemavu wilayani humo kufanya kazi kwa bidii badala ya kukaa nyumbani na kutegemea misaada kutoka kwa wadau jambo ambalo sio zuri.

Naye Ofisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, Husna Lumaliza, aliwataka wanakikundi hao kutumia fursa ya kupata mikopo ya halmashauri ambayo itaanza kutolewa Julai mwaka huu.

Alisema mifumo ya utolewaji mikopo imewekwa vizuri kuwa ya kisasa tofauti na zamani.

# Bil.3.3/- kujenga vyoo, uboreshaji huduma za maji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKOA wa Mbeya umepokea zaidi ya Sh. bilioni 3.377 kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa vyoo bora na uboreshaji wa huduma za maji kwenye maeneo ya umma.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera aliyasema hayo alipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa miundombinu hiyo katika Zahanati ya Mbugani wilayani Chunya.

Alisema miradi hiyo inatekelezwa kupitia mradi wa WASH ambao unafadhiliwa na Benki ya Dunia (WB).

Alisema katika Mkoa wa Mbeya mradi huo unatekelezwa katika halmashauri tano kati ya saba na kwamba ni halmashauri za Rungwe na Busokelo pekee ndizo hazikupatiwa fedha.

Alisema ili kuhakikisha mradi huo unatekelezwa vizuri kwenye mkoa huo, wanakusudia kuandaa vyeti na tuzo kwa viongozi wote watakaosimamia vizuri hasa waganga wakuu wa halmashauri na maofisa afya.

"Lakini kati ya fedha hizi Halmashauri ya Chunya ndiyo iliyopata fedha nyingi ambazo ni Sh. bilioni 1.3 kwa hiyo lazima msimamie vizuri ili matokeo yanayokusudiwa yapatikane," alisema Homera.

Aliwasisitiza viongozi wa wilaya zote za mkoa huo kuhakikisha kwenye maeneo yote ya umma ikiwamo kwenye vituo vya mabasi wanajenga miundombinu hiyo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Bosco Mwanginde, aliishukuru serikali kwa kuipatia halmashauri hiyo fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo kwa maelezo kuwa zitasaidia kuboresha huduma kwa wananchi.

Alisema Zahanati ya Mbugani ni miongoni mwa zahanati ambazo zilikuwa na hali mbaya kutokana na kukosa miundombinu muhimu na kwamba ukarabati uliofanywa utasaidia wananchi kupata huduma nzuri kama ilivyo kwenye maeneo mengine.

Aliwashukuru pia watendaji wa halmashauri hiyo kwa kusimamia vizuri mradi huo akidai kuwa kwa sasa wananchi watakuwa wanapata huduma kwenye eneo ambalo lina sifa nzuri.

Akitoa taarifa ya ujenzi wa miundombinu ya zahanati hiyo, Mhanga Mkuu wa Halmashauri ya Chunya, Dk. Dauson Andrew alisema wamejenga miundombinu ya maji, ujenzi wa vyoo bora, eneo la kunawia na kichomea taka.

Alisema kwa sasa wanaendelea na utekelezaji wa mradi huo katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo ili kuhakikisha huduma za afya zinaboreshwa kwa wananchi.



# Makamu wa Rais awapa majukumu matatu mawaziri biashara Afrika

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, amewataka mawaziri wa biashara Afrika kuweka mikakati imara itakayosaidia kuunganisha Afrika, kukuza biashara za ndani.

Aliyasema hayo jana visiwani Zanzibar wakati akifungua mkutano wa 14 wa mawaziri wa biashara wa eneo huru la biashara Afrika.

Alisema kuwapo kwa eneo huru la biashara ni hatua muhimu ya mwelekeo sahihi katika kutimiza ndoto za viongozi ambao walipigania ili kuhakikisha Afrika inajitegemea kiuchumi.

Hemed alisema Afrika inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo kukosekana kwa usalama wa baadhi ya maeneo, ukosefu wa nishati ya kutosha, miundombinu ya barabara, reli na usafiri wa anga, uzalishaji mdogo pamoja changamoto ya mawasiliano kutokana na kuwapo kwa lugha nyingi miongoni wa wananchi.

Aidha, alisema eneo lingine la kujikita ni kuwezesha biashara ndogo na za kati zishiriki kikamilifu katika biashara za kikanda na kimataifa pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa mikopo nafuu, elimu ya biashara na makosa.

Alisema pia kuhakikisha ushirikiano wa kikanda ambao ni muhimu kwa mafanikio ya eneo huru la biashara la Afrika, kupunguza urasimu, kuimarisha utawala bora, kuhakikisha usalama wa mitaji na mali za wawekezaji ambapo kufanya hivyo kutasaidia kuvuta wawekezaji.

Hata hivyo, alisema Jamhuri ya Muunano wa Tanzania iko tayari kushirikiana na nchi zote wanachama wa eneo huru la biashara la Afrika katika kufanikisha malengo yaliyowekwa.

Waziri wa Biashara na Viwanda, Omar Said Shabani alisema, wamejadiliana na masuala muhimu katika biashara Afrika ikiwamo mabadiliko ya hali ya hewa na mapinduzi ya kijani ya maendeleo ya viwanda.

Aidha, alisema wamezungumzia fursa zilizopo katika uzalishaji wa vipuri vya magari ili kunufaika na biashara katika sekta ya magari ambayo ni sekta inayokuwa kwa kasi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Uwekezaji, Shari Ali Saharif, alisema Rais Dk. Samia Suluhu na Dk. Hussein Ali Mwinyi ni viongozi mashuhuri na shupavu.

Alisema pia ni watetezi wa dhati wa ushirikiano na kiuchumi na maendeleo kote Afrika.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, akizungumza wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa 14 wa Mawaziri wa Biashara wa Eneo Huru la Biashara la Afrika, Mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Dk. Mwinyi mgeni rasmi Siku ya Sheria

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

MAADHIMISHO ya Siku ya Sheria Duniani yanatarajia kufanyika Juni 28 mwaka huu visiwani Zanzibar, mgeni rasmi akitarajiwa kuwa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Akizungumza na waandishi habari, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, alisema kauli mbiu ya maadhimisho hayo ni kuhakikisha haki inapatikana kwa urahisi kupitia teknolojia.

Alisema kauli mbiu hiyo imetokana na uwepo wa mabadiliko ya teknolojia duniani na kuimarika kwa huduma za msaada wa kisheria.

Alisema huduma hizo za msaada wa kisheria zinapatikana kwa urahisi kupitia njia ya teknolojia, hivyo kuendana na mabadiliko hayo na uhitaji mkubwa kwa jamii.

Aidha, alisema maadhimisho hayo yatajumuisha shughuli mbalimbali visiwani Unguja na Pemba ikiwamo kampeni ya vyombo vya habari kuhusu Wiki ya Msaada wa Kisheria.

Alisema pia kutakuwa na kongamano la vyuo vikuu kuhusu masuala ya msaada wa kisheria, utoaji wa msaada wa kisheria kwa kaya maskini na kwenye vituo vya polisi.

Maadhimisho hayo ya siku ya msaada wa kisheria yameratibiwa na idara ya katiba na msaada wa kisheria kwa kushirikiana na Shirika la Msaada wa Kisheria Tanzania (LSF) pamoja na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP).

## Serikali yatoa ufafanuzi yalipo majenereta ya kufua umeme

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WIZARA ya Maji, Nishati na Madini imesema ni kweli kwamba Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) lilikuwa linamiliki majenereta matano ambapo kati yao matatu yalikuwa Pemba na mawili yalikuwapo Unguja.

Imesema majenereta hayo yalikuwa yakitumika kwa ajili ya kufua umeme kwa kutumia mafuta mazito (IDO) kabla ya visiwa hivyo kuunganishwa na gridi ya taifa kupitia waya za baharini kutoka Tanga - Pemba na Kiromoni - Fumba Unguja.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Wizara hiyo, Hassan Kaduara katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali aliloulizwa na mwakilishi wa Pandani, Profesa Omar Fakihi aliyetaka kujua jenereta hizo ziko katika hali gani kwa sasa na zinatumika kwa matumizi gani.

Alisema Kisiwa cha Unguja kiliunganishwa kwenye gridi mwaka 1980 na hivyo kupunguza kwa kiwango kikubwa matumizi ya majenereta hayo. Alisema kwa upande wa Pemba majenereta yaliendelea kutumika mpaka kufikia mwaka 2011 ambapo yalizimwa kabisa baada ya kisiwa hicho kuunganishwa na gridi ya taifa kutokea Tanga.

Alisema kuwa jenereta hizo tano zilishatumika kwa kipindi kirefu na hivyo kupelekea uwezo wake wa kutoa huduma na upatikanaji wake wa vipuri kuwa mgumu na wenye gharama kubwa.

Alisema shirika liliandikia Ofisi ya Msajili wa Hazina kuomba kufanyiwa utaratibu wa kuziondoa kama utaratibu wa serikali unavyoelekeza.

"Naomba kulijulisha baraza lako tukufu kwamba kwa mamlaka aliyopewa kwa mujibu wa sheria, Msajili wa Hazina amekamilisha zoezi la uuzaji wa jenereta hizo tano na taarifa rasmi imeshawasilishwa kwenye Shirika la Umeme Zanzibar," alisema.

Waziri Kaduara alisema kuhusiana na jenereta tano zinazomilikiwa na Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) ambazo shirika liliomba kuzifanyia matengenezo ili ziweze kutumika kwa kazi mbalimbali za dharura itakapohitajika zipo kwenye Kituo cha Umeme Mtoni zikifanyiwa matengenezo.

Alisema zitakapokamilika zitaanza kutumika kama ilivyokusudiwa na ambazo hazitawezekana matengenezo yake zitarudishwa kwa mmiliki wake ambaye ni Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA).

Akizungumzia mpango wa serikali wa kupambana na hali ya dharura ya umeme endapo kutakuwa na ukosefu ama upungufu wa umeme kutoka Tanzania Bara, alisema serikali imefanya jitihada za kuhakikisha kuwa inaweka vyanzo vya umeme katika Kisiwa cha Unguja na Pemba.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**DESTINATION STEPHANO MBILINYI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1157/0062** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **SHULE YA SEKONDARI IWAWA** mwaka **2016** kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: PHQ/MOR/KIL/6617/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ELISHA JOHN MARWA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S2693/0022 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MWANDEGE BOYS' SECONDARY SCHOOL** mwaka 2020. Kwa yeyote atakaeiona ato taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA : PHQ/DAR/ILA/125523/2024**

**IN THE DISTRICT COURT OF MWANGA**
**AT MWANGA**
**MATRINMONIAL CAUSE NO 14004 OF 2024**
**HENRISH ALLAN MWANGA ......PETITIONER**
**VERSUS**
**MAGRETH PASCHAL MNEO...RESPONDENT**

**NOTICE OF MENTION**

**TAKE NOTICE** That the above case has been fixed for mention on 28th day of June, 2024 at 9:00am before Honourable A.S. HAYATA-RM.
YOU ARE Required to appear in this District of Mwanga without fail and you must produce to that day all documents upon which you intended to rely in support of your case.
GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THIS COURT This 24th day of June, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE
MWANGA DISTRICT
Resident Magistrate
Mwanga

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA [W] BOMANI**
**KUITWA SHAURINI**
**[MCA 84]**
**SHAURI LA MADAI NAMBA 67.2024.**
**MDAI...........LEONARD LONE LUKANSOLA.**
**DHIDI YA MDAIWA.......KAMPUNI YA LOTUS VALLEY LIMITED**

**Kwa:KAMPUNI YA LOTUS VALLEY LIMITED**
Mdaiwa popote ulipo Shauri la madai tajwa hapo juu limefunguliwa katika mahakama hii leo tarehe 14/06/2024 na shauri hili limepangwa kutajwa tarehe 12/07/2024 saa 2:30 asubuhi. Hivyo basi unatakiwa wewe mdaiwa kuhudhuria hapa mahakamani siku hiyo bila kukosa. Usipofika shauri hili litaendelea kusikilizwa upande mmoja na kutolewa uamuzi wa upande mmoja. Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa mahakama hii leo tarehe 24/06/2024.

RESIDENT MAGISTRATE
Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo

## KUPOTEA KWA CHETI



**ANTHONY KYARUZI** anatangaza kupotea kwa cheti cha DIPLOMA IN COMMUNITY DEVELOPMENTchenye usajili namba DCD 02/59/2008 kilichotolewa na MONDULI COMMUNITY DEVELOPMENT TRAINING INSTITUTE mwaka 2010. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIN/125650/2024**

## RENTAL AND SALE OF PLANT AND EQUIPMENTS (SLAUGHTER HOUSE OR ABATTOIR)

The existing beef and mutton Slaughtering and processing plant has a full set of production lines and cool storage for rent, located in the capital City of Dodoma with an area of 5,000 square meters and convenient transportation, which can be used for the production of all products and storage of beef and mutton. In addition, there is an idle standard warehouse of 10,000 square meters for rent, with a height of 12 meters.
Processing plant equipment: Generator sets, refrigeration equipment, cold storage, dried meat production lines ovens, fryers, spin dryers, automatic vacuum packaging machines, gas storage tanks, hot water tanks, tumbling machines, beef jerky slices, hair removal machines, packaging machines and other equipment for rent and sale.
Interested parties can contact us in the following ways.

**Contact numbers (Whatsapp) :-**
**0714424623/0715315881/0745115678**

## KUPOTEA KWA VYETI



**ANTHONY KYARUZI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0586-0031 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia KAISHO SECONDARY SCHOOL mwaka 2005, cheti cha chuo cha CERTIFICATE COURSE IN COMMUNITY DEVELOPMENT chenye usajili namba BCC/CD No 26/2473 kilichotolewa na BUHARE MUSOMA COMMUNITY DEVELOPMENT TRAINING INSTITUTE mwaka 2008. Wa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIN/125653/2024**

**THE JUDICIARY OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT COURT OF MBINGA**
**AT MBINGA**
**EXECUTION NO. 2886/2024**
**AMSEK SECURITY SERVICE LTD..........DECREE HOLDER**
**VS**
**CHINA HENAN INTERNATIONAL COOPERATION GROUP C.O. LTD (CHICO) .........JUDGMENT DEBTOR**
**KWA: CHINA HENAN INTERNATIONAL COOPERATION GROUP C.O LTD. (CHICO)**
**NOTICE OF HEARING**

**TAKE NOTICE** That the above suit has been set down for mention on the **08** day of **April 2024** at **08:30 am** in the forenoon thereafter.

Given under my hand and the seal of the Court this **25** day **March** of **2024**

**L.B MWAPEMELA**
**RESIDENT MAGISTRATE**
**MBINGA**

## KUPOTEA KWA CHETI



**TOBALDINA KALIST KASIAN** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S4808-0027, kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia EMBEKO SECONDARY SCHOOL mwaka 2020 kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA:PHQ/DOD/CHA/25880/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ERASTO ANAEL ABRAHAM**
anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili T153DAX aina ya Nissan Caravan yenye Chasis namba VWE25050305 na Engine namba ZD30029476.
Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/MAN/BAB/4766/202**

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO. 13489 OF 2024**

**In the Matter of the Estate of the Late:**
**BERTHA MGONYA NYABANGE**

**By 1: LUCAS WILSON NYABANGE**
**2: ____________________**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 15 day of 7.2024
Dated at MOROGORO this 21 day of 6.2024

RESIDENT MAGISTRATE

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku
Piga Simu 0677020701

OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0677020701
E-mail: advertise@guardian.co.tz,
Website: www.ippmedia.com

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Hali bado tete maandamano Kenya

## •10 wauawa, 200 wajeruhiwa •Biashara, barabara zafungwa

**NAIROBI,** Kenya



Vijana nchini Kenya wakiandamana barabarani jana huku wakiwa wamenyoosha mikono juu na kuonyesha alama ya X ishara ya kupinga muswada wa fedha. **PICHA: MTANDAO.**

HALI ya maandamano nchini Kenya bado imeendelea kuwa kitendawili huku wahudumu wa afya wakieleza kuwa waandamanaji 10 wameuawa baada ya kuingia tena barabarani jana kwa lengo la kupinga muswada wa fedha licha ya Rais William Ruto kusema yuko tayari kuzungumza nao.

Inaelezwa kuwa makabiliano makali yalizuka jana katikati ya mji wa Nairobi baada ya polisi kukabiliana na waandamanaji wanaopinga muswada wa fedha wa 2024.

Katika makabiliano hayo ilibainishwa kuwa karibu waandamanaji 200 walijeruhiwa, na kwamba 45 kati yao walipelekwa kwenye hospitali ya Kitaifa ya Kenyata huku 100 wakikamatwa na polisi.

Pia picha za Televisheni za moja kwa moja zilionesha sehemu ya bunge ikiwa imeharibiwa vibaya, madirisha na viti vikionekana vimevunjwa huku polisi wakiendelea kuwasukuma nje waandamanaji walioifikia jengo hilo.

Ilielezwa kuwa umati wa waandamanaji uliobeba mabango na kuimba nyimbo za kuikashifu serikali ulianza kukusanyika katika maeneo mbalimbali ya mji wa Nairobi kuanzia saa moja alfajiri jana.

Maandamano hayo yanayoshirikisha vijana wa Gen Z waliojihami kwa maji na kamera za simu kuonesha msimamo wao dhidi ya muswada huo, waliandamana wakati bunge likiwa linajadili marekebisho ya muswada huo wa fedha.

**BUNGENI**

Ilibainishwa kuwa wabunge wa upinzani ambao awali walikuwa wamewasilisha mapendekezo ya kurekebisha muswada huo, walifutilia mbali marekebisho hayo na kutaka muswada huo kukataliwa wote kwa jumla.

Pia ilielezwa kuwa muswada huo ulipita awamu ya pili wiki iliyopita baada ya wabunge 204 kuunga mkono huku 115 wakipinga. Na kwamba baada ya hapo utasogea awamu ya tatu ambako Bunge litaupigia kura ukiwa na marekebisho mapya.

Aidha, taarifa zinaeleza kuwa maandamano hayo yalijiri huku shughuli za biashara katikati ya mji mkuu wa Kenya zikisitishwa kwa sababu ya kufungwa kwa idadi kubwa ya maduka na shughuli zingine.

Hata hivyo, juzi serikali ilionya Wakenya waliopanga kuandamana jana dhidi ya aina yoyote ya ghasia na uharibifu wa mali.

Waziri wa Mambo ya Ndani, Kithure Kindiki, mbali na kukiri kwamba kila Mkenya ana haki ya kuandamana au kulaani, alisisitiza kwamba waandamanaji hawapaswi kukiuka haki na uhuru wa wengine.

**BARABARA ZAFUNGWA**

Katika hatua nyingine, ilibainishwa kuwa barabara katika mji mkuu wa Nairobi zilifungwa kabla ya maandamano ya kupinga muswada wa sheria ya fedha kuanza.

Ilielezwa kuwa maofisa wa usalama nchini humo, walifunga barabara kadhaa muhimu zinazoelekea kwenye majengo ya Bunge zikiwemo 'Parliament Road' na 'City Hall Way' na kutoruhusu magari na watembea kwa miguu kupita huku hatua za usalama zikizidi kuimarishwa. Vile vile, ilielezwa kuwa magari ya polisi ya kuzima ghasia na lori ziliwekwa katika barabara hizo kama vizuizi katika njia kuu zinazoelekea bungeni.

Maandamano hayo, yaliyoandaliwa na mashirika mbalimbali ya kiraia yamevutia uungwaji mkono mkubwa kutoka kwa vijana kote nchini humo.

Waandaaji wa maandamano hayo, vijana ambao wanafahamika kama Gen Z pia walitoa wito kwa zaidi ya watu milioni moja kujitokeza na kushiriki.

Maandamano hayo yaliyopewa jina la 'Kenya Reject-Finance Bill 2024' ikiwa na maana ya kupinga muswada wa fedha wa 2024, yalikuwa yakishika kasi na kuvutia maelfu ya watu mitaani kuonyesha upinzani wao.

Vijana hao walihoji kuwa mpango wa kukusanya kodi zinazopendekezwa katika muswada huo zitazidisha hali ngumu ya kiuchumi kwa Wakenya wa kawaida.

***BBC***

# TANROADS na TARURA zaonywa kuacha vifusi, viraka barabarani

**Na Halfani Chusi**

SERIKALI imeonya kitendo cha baadhi ya wafanyakazi wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kurundika vifusi barabarani na kuvitelekeza bila sababu maalum.

Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Miundombinu katika Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Rogatus Mativila, alitoa onyo hilo juzi jijini Dar es Salaam wakati akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo viongozi wa serikali na wadau wa sekta za ujenzi.

Mafunzo hayo yanalenga matengenezo ya barabara yatakayozingatia usalama wa watumiaji.

Mativila alisema kifusi kinachorundikwa barabarani hakipaswi kuzidi saa 48 wala kubugudhi wapitanjia.

"Utaratibu huu tunapiga vita sana na yeyote atakayebainika amerundika kifusi kwa muda mrefu tutamchukulia hatua kali za kisheria, tunataka kuona ndani ya saa 48 kifusi kimeshafanyiwa kazi, tunaomba wananchi wakiona hali hiyo watoe taarifa," alionya.

Mativila pia alikemea kitendo cha wale wanaochonga kipande cha barabara kwa lengo la kuweka kiraka na kukiacha kwa muda mrefu bila marekebisho, huku akiahidi kuyafanyia kazi maadhimio na mapendekezo yatakayotokana na mafunzo hayo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Mpango wa Usalama Barabarani (TARSI), Maliki Balongo, ambao ni waandaji wa mafunzo hayo, alisema lengo ni kusaidia serikari kupunguza ajali za barabarani zinazosababishwa na ubovu wa miundombinu.

Alitaja lengo lingine la mafunzo hayo ni kutoa elimu ya usalama barabarani kwa makundi yote ya watumiaji ili wazingatie ubora wa viwango vinavyotakiwa ikiwamo alama za usalama.

"Mwaka huu kumekuwa na mvua kubwa ambayo imesababisha uharibifu wa barabara, tumeona ajali nyingi zimetokea, kuna haja kuandaa mafunzo haya ili pale ambapo pana shida parekebishwe yasitokee madhara makubwa," alisema Balongo.

Mhandisi Mwandamizi Delophina Mhagama kutoka TANROADS, alisema mafunzo hayo yatawasaidia katika mambo mengi, ikiwamo kujua namna ya kulinda usalama wa watumiaji barabara na kuepusha ajali zinazotokana na kutoziba kwa wakati mashimo.

Ally Ismail kutoka TARURA alisema mafunzo hayo ni muhimu katika sekta zinazosimamia barabara kwa kuwa yanagusia namna ya kuzitengeneza zitakazodumu kwa muda mrefu na kuondokana na ajali.

# Serikali yaahidi uwekezaji zaidi kidijitali sekta elimu

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imesema imedhamiria kuendelea kuwekeza kidijitali ili kuharakisha mageuzi katika sekta ya elimu nchini.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo, aliyasema hayo jana katika ufunguzi wa mjadala kuhusu rasimu ya mkakati wa kitaifa wa matumizi wa teknolojia za kidijitali katika elimu.

Katika mjadala huo, Prof. Carolyne aliwaomba wadau wa maendeleo pamoja na sekta binafsi kushirikiana na serikali kuwekeza kwa kuzingatia mipango na vipaumbele shirikishi katika sekta hiyo.

"Serikali kupitia wizara yenye dhamana ya elimu iliona haja ya kuwa na mkakati wa matumizi ya teknolojia za kidijitali katika elimu na katika kufanikisha hilo. Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa) na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, iliunda kikosi kazi na kukipa jukumu la kuandaa rasimu ya mkakati husika.

"Baada ya kukamilika kwa rasimu ya mkakati, menejimenti ya wizara na kamati ya pamoja ya wizara tatu yenye dhamana ya kuratibu na kushauri serikali kuhusu masuala ya teknolojia za kufundishia na kujifunzia, iliridhia mkakati husika uletwe kwa ajili ya kujadiliwa na kupata maoni ya makundi mbalimbali ya wadau," alisema.

Prof. Carolyne alisema uwapo na ushiriki wao katika mjadala huo wa kitaifa ni hatua muhimu kuelekea katika mageuzi ya elimu wanayoyatamani.

Alisema mkakati huo ndio utatoa fursa kwa nchi kuandaa miongozo mahsusi kuhusu matumizi ya teknolojia za kidijitali nchini ikiwamo mwongozo wa matumizi ya Akili Mnemba (Artificial Intelligence) katika ufundishaji na ujifunzaji.

Prof. Carolyne alisema TEHAMA na teknolojia nyingine za kidijitali ni nyenzo muhimu katika mageuzi ya sekta ya elimu ambayo serikali inayadhamiria ambayo yatasaidia mkukiabiliana na changamoto mbalimbali katika sekta ya elimu nchini ikiwamo uchache wa miundombinu, walimu pamoja na rasilimali nyingine.

"Sera na mitaala iliyoboreshwa sio tu inasisitiza kuongeza matumizi ya TEHAMA na teknolojia nyingine katika elimu, bali inasisitiza kuzalisha rasilimali watu yenye maarifa na ujuzi wa kutumia na kubuni teknolojia zinazoakisi mahitaji na changamoto za nchi na dunia kwa ujumla.

# MWAMNYETO ATAJWA KUMRITHI INONGA SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kumpiga bei beki wake tegemeo, Henock Inonga, Klabu ya Simba imesema tayari imeshampata mbadala wake ambaye watamtangaza hivi karibuni, huku nahodha wa Yanga, Bakari Mwamnyeto, akihusishwa kujiunga na 'Wekundu wa Msimbazi' hao.

Akizungumza jana, Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, alisema walifahamu siku nyingi kuwa Inonga ataondoka, hivyo kabla hata Ligi Kuu msimu uliomalizika haijaisha walikuwa wameshapata beki mwingine wa kuziba pengo hilo.

"Tulijua siku nyingi kuwa Inonga anaondoka, kwa hiyo wakati tunamalizia mechi za mwisho tayari tulikuwa tumeshapata mrithi wake, kwa hiyo niwaambie tu kuwa mrithi wake ameshapatikana, ni beki kitasa mwenye uwezo mkubwa, kama unamuondoa Inonga tafsiri yake ni kwamba lazima umlete wa kulingana naye au zaidi, tayari tumeishaipata hiyo mashine, muda si mrefu tutakwenda kumtambulisha, wanachama na mashabiki wa Simba wawe na subira," alisema Meneja Habari huyo.

Wakati Ahmed akijinasibu kumpata mrithi wa Inonga, taarifa zinadai klabu hiyo ipo kwenye mazungumzo na Mwamnyeto ambaye inasemekama mpaka sasa bado hajasaini mkataba mpya na Yanga.

Meneja wa mchezaji huyo aliyejitambulisha kwa jina la Carlos 'Master Mind', amekiri kuwa ofa ya Simba iko mezani na nzuri, ila muda ndiyo utaongea.

"Ni suala la muda ukifika tutajua mustakabali, maongezi na Yanga yanakwenda vizuri sioni kama kuna changamoto yoyote, ila bado hatujamalizana nao, ofa ya Simba nayo ipo mezani na ni nzuri pia, tunaitafakari.

unapoongea ofa za hizi klabu mbili kubwa huwa hazipishani sana, kitu ambacho Yanga anaofa, sidhani kama Simba washindwa na Simba nao wakifanya hivyo Yanga hashindwi pia, kikubwa ni utayari wa mchezaji mwenyewe wapi anaona ni sahihi kwenda kufanya kazi," alisema meneja wa mchezaji huyo.

Hata hivyo, zipo taarifa zingine kuwa mbali na Mwamnyeto kutaka kwenda kuvaa viatu vya Inonga, Simba pia inatajwa kumshusha beki wa Asec Mimosas ya Ivory Coast, Anthony Tra Bi Tra.

Akizungumzia kuondoka kwa Inonga, Ahmed amesema wamemuuza kwa kiasi ambacho ni siri kati ya Simba na klabu yake mpya, FAR Rabat ya Morocco.

"Tumemuuza Inonga, kiasi cha pesa kinabaki kuwa siri kati ya Simba na FAR Rabat, tunamtakia kila la kheri.

"Simba imenufaika sana na dili hili ikizingatiwa kuwa wenyewe Wamorocco ndiyo walikuwa wanamhitaji, sokoni sisi tukawa na nguvu kubwa tukapanda bei, tukamuuza kwa pesa nzuri kwa sababu alibakisha mkataba wa mwaka mmoja na sisi," alisema.

Vyanzo vinasema Simba imemuuza kwa kiasi cha Dola 200,000 za Kimarekani ambazo ni sawa na kiasi cha Sh. milioni 522.3 za Tanzania ambazo FAR Rabat wametoa ili kuvunja mkataba.

Inonga anayecheza beki wa kati anayeichezea pia Timu ya Taifa ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, anaondoka Simba akiwa amecheza kwa misimu mitatu, katika klabu hiyo iliyokuwa imesajili kutoka DC Motema Pembe ya DR Congo.

## Tondo ampania Mchanjo 'Dar Boxing Derby'

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA Charles Tondo amejitapa vikali kumchapa mpinzani wake Haidary Mchanjo katika pambano la 'Dar Boxing Derby' litakalofanyika Juni 29, mwaka huu, kwenye viwanja vya Posta vilivyopo Kijitonyama, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, bondia huyo alisema mpinzani wake hamuumizi kichwa kwani anamfahamu vizuri.

"Mchanjo ajipange, sitakuwa na huruma siku hiyo nataka nimfundishe Mchanjo jinsi ngumi zinavyopigwa na si kupiga kelele," alisema Mchanjo.

Alisema hana maneno mengi bali ataonyesha vitendo akiwa ulingoni, na kuahidi kuwapa burudani mashabiki wake.

Aidha, alimshukuru mwandaaji wa pambano hilo, Meja Selemani Semunyu kwa kazi kubwa anayoifanya kuhakikisha mchezo wa ngumi unakua.

"Ninamshukuru Meja Semunyu kwa msaada mkubwa anaotufanyia sisi vijana kwani tunapata riziki vile vile tunajitangaza kupitia mapambano anayoyaandaa," alisema bondia huyo.

Aliwataka vijana kujifunza mchezo wa ngumi kwani unawasaidia kupata ajira pamoja na kuimarisha afya zao kutopata magonjwa kirahisi.

## Tibarazwa na siri ushindi kuogelea

**Na Shufaa Lyimo**

MWOGELEAJI wa Timu ya Taifa ya Kuogelea ya Tanzania, Mark Tibarazwa, amesema siri ya ushindi wake kwenye mashindano ya kimataifa yaliyomalizika jijini Nairobi nchini Kenya wiki iliyopita, ni kufuata vema maelekezo anayopewa na kocha wake pamoja na nidhamu.

Akizungumza na Nipashe jana, Tibarazwa alisema licha ya kufanikiwa kupata medali nane, mashindano yalikuwa magumu kwani amezoea kuogelea kwenye bwawa la mita 25.

"Mashindano yalikuwa magumu kwani niliogelea kwenye bwawa la mita 50 tofauti na nyumbani nilizoea la mita 25 ila ninashukuru kwa ushindi niliyoupata," alisema Tibarazwa.

Alisema mazingira yalikuwa si mazuri kutokana na hali ya hewa kuwa ya baridi tofauti ya Dar es Salaam ambayo wameizoea.

Tibarazwa alisema alipambana kufa kupona kuhakikisha anaipeperusha vema bendera ya Taifa kupitia mashindano hayo jambo ambalo alifanikiwa.

Aliongeza kuwa malengo yake ni kuwa mwogeleaji wa kulipwa nje ya nchi, ikiwa ni ndoto yake ya muda mrefu.

VITANI!...




Beki wa kati wa Croatia, Josip Sutalo, akiokoa hatari langoni mwao huku mshambuliaji wa Italia, Mateo Retegui, akiingiza kichwa wakati wa mechi ya Kundi B ya michuano ya Euro 2024, iliyopigwa juzi nchini Ujerumani na kumalizika kwa sare ya bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

## MAKATA KOCHA MKUU PRISONS

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Prisons imemtangaza aliyekuwa Kocha Mkuu wa Pamba, Mbwana Makata, kuwa ndiye atakayekinoa kikosi hicho kwa msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano mengine.

Katibu Mkuu wa Klabu hiyo, Ajibu Kifukwe, amesema wamemchukua kocha huyo kutokana na uzoefu wake katika soka la Tanzania, akiwa amezifundisha klabu nyingi za Ligi Kuu na Ligi ya Championship.

Prisons imemtangaza kocha huyo jana, huku wakimwacha aliyekuwa kocha wao, Ahmad Ally, ambaye anaondoka kwenye klabu hiyo, huku taarifa zikisema anakwenda kuwa Kocha Mkuu wa JKT Tanzania kuchukua nafasi ya Malale Hamsini.

"Tunapenda kuwataarifu mashabiki wa Prisons kuwa Makata ndiye Kocha Mkuu wetu msimu ujao, ni mtaalam na kocha mzoefu wa soka la Tanzania," alisema Kifukwe.

Kocha huyo anatua kwenye kikosi hicho siku chache baada ya kuonyeshwa mlango wa kutokea na Klabu ya Pamba FC, ambayo ameipandisha daraja kutoka Ligi cha Championship hadi Ligi Kuu na baada ya hapo imemtwaa Goran Kopunovic kuwa kocha wao.

Makata alikiongoza kikosi cha Pamba kucheza mechi 30, kikishinda 20, sare saba na kupoteza mechi tano, kikivuna pointi 67 na kushika nafasi ya pili kwenye Ligi ya Championship msimu uliomalizika.

"Kwa makubaliano ya pande zote mbili, timu ya Prisons tumefikia muafaka wa kuachana na kocha wetu, Hamad.

"Tumezingatia maslahi ya pande zote mbili na klabu inamshukuru kwa mchango wake katika kipindi chote alichokuwa akifundisha timu yetu, tunamtakiwa kila la kheri katika safari yake ya soka," alisema Katibu Mkuu huyo.

Hamad alikichukua kikosi cha Prisons katikati ya msimu wa ligi iliyomalizika kikiwa kwenye nafasi ya chini huku wengi wakidhani kuwa kinaweza kushuka daraja, akakiongoza vema kwenye mzunguko wa pili kwa mafanikio, kwa kukiwezesha kumaliza nafasi ya tisa, kikifikisha pointi 34.

## ZISIKUPITE

### ZIRKZEE NA MAN UNITED

MANCHESTER United inatazamia kukidhi kipengele cha kuruhusiwa kuondoka kwa Joshua Zirkzee huku wakipanga kumuuza Mason Greenwood ili kufadhili mpango huo, nao Everton wakitakiwa kuwasilisha ombi jingine kwa Jarrad Branthwaite. ***(Mail)***

### BRANTHWAITE OFA NYINGINE

KLABU ya Everton inatarajia Manchester United itawasilisha ofa nyingine kwa beki wa England, Jarrad Branthwaite, 21. ***(Liverpool Echo)***

### NDIAYE ANUKIA EVERTON

EVERTON inakaribia kufikia makubaliano ya kumsajili mshambuliaji wa Senegal, Iliman Ndiaye mwenye umri wa miaka 24, kutoka Marseille. ***(Footmercato)***

### TEN HAG MKATABA MPYA

MANCHESTER United inatarajia kukubaliana mkataba mpya na Kocha Erik ten Hag, kabla ya kuanza kwa ziara yao ya kujiandaa na msimu mpya nchini Marekani mwezi ujao. ***(ESPN)***

### NISTELROOY KUMSAIDIA HAG

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Manchester United, Ruud van Nistelrooy mwenye umri wa miaka 47, amefanya mazungumzo chanya kuhusu kurejea katika klabu hiyo kama sehemu ya wasaidizi wa Erik Ten Hag. ***(Talksport)***

### OSIMHEN SASA KUUZWA

KLABU ya Napoli itazingatia ofa ya kiwango cha euro milioni 100 kwa mshambuliaji wa Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 25, na mshambuliaji wa Chelsea na Ubelgiji, Romelu Lukaku anatarajiwa kuchukua nafasi yake. ***(Calciomercato)***

### JOSELU KUONDOKA MADRID

MSHAMBULIAJI wa Hispania, Joselu mwenye umri wa miaka 34, anakaribia kuondoka Real Madrid baada ya kupokea ofa kutoka kwa Klabu ya Qatar, Al Gharafa. ***(Athletic)***

### GULU AWANIWA CHELSEA

CHELSEA imeanza mazungumzo na Barcelona kuhusu mkataba wa kumnunua mshambuliaji wa Hispania, Marc Guiu, 18. ***(ESPN)***

### GRAY ATAJWA DORTMUND

KLABU ya Borussia Dortmund inavutiwa na kiungo wa kati wa Leeds United, Archie Gray, 18. ***(Bild)***

### DAVID ANYATIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur imeanza mazungumzo na wawakilishi wa mshambuliaji wa Lille na Canada, Jonathan David mwenye umri wa miaka 24, ambaye pia anahusishwa na kuhamia Chelsea. ***(Football Insider)***

### KUDUS ATAKA KUONDOKA

MCHEZAJI wa Ghana, Mohammed Kudus mwenye umri wa miaka 23, amekuwa akihusishwa na kutaka kuondoka West Ham, lakini klabu hiyo bado haijapokea ofa ya kiungo huyo mshambuliaji. ***(Sky Germany)***

DO A SOKA
MA ULAYA



# MODRIC: BADO NATAKA KUENDELEA KUCHEZA TU

●●●Ningependa kucheza milele, lakini pengine itakuja wakati ambapo ni lazima nitunze...

**BERLIN,** UJERUMANI

NAHODHA wa Croatia, Luka Modric, amesema ataendelea kucheza licha ya nchi yake kuondolewa kwenye michuano ya Ulaya baada ya kuruhusu bao la dakika za lala salama katika sare ya 1-1 na Italia katika mchezo wao wa mwisho wa Kundi B Jumatatu.

Modric, mshindi wa tuzo ya Ballon d'Or mwaka 2018 wakati Croatia ilipotinga fainali ya Kombe la Dunia mjini Moscow, aliiweka timu yake mbele sekunde za mwanzo, lakini akatazama kwa mshtuko baada ya kutolewa nje huku Mattia Zaccagni wa Italia akifunga bao la kusawazisha kwa mkwaju wa dakika za majeruhi.

Sare hiyo iliiweka Italia katika hatua ya 16-bora na kuiacha Croatia katika nafasi ya tatu katika Kundi B ikiwa na pointi mbili - ambazo hazikuweza kutosha kuchukua moja ya nafasi zilizohifadhiwa kwa washindwa wanne bora (best loser) walio katika nafasi ya tatu.

Licha ya kukatishwa tamaa, Modric alipendekeza alitaka kuendelea hata baada ya mechi 178 za kimataifa tangu alipoanza kucheza mwaka 2006 na lengo lake likimfanya kuwa mfungaji mwenye umri mkubwa zaidi kuwahi kucheza Euro.

"Ningependa kuendelea kucheza milele, lakini pengine itakuja wakati ambapo ni lazima nitunze buti zangu. Nitaendelea kucheza, lakini sijui kwa muda gani," alisema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 38 akiwaambia waandishi wa habari.

"Hiyo ilikuwa ya kusisitiza sana," alisema. „Tuliendelea kupambana hadi mwisho, lakini kwa bahati mbaya, soka halikuwa na huruma na sisi usiku wa leo. Ulikuwa wa kikatili, lakini katika mechi yetu ya mwisho sare ya 2-2 na [Albania] tuliporuhusu pia bao la dakika za lala salama.

"Lakini hiyo ni sehemu ya soka. Mara nyingi hukupa tabasamu nyingi, lakini nyakati nyingine inakuhuzunisha sana kama ilivyokuwa leo, kupoteza kwa jinsi tulivyofanya."

HABARI MICHEZO

# UNITED YAKOMAA USAJILI WA ZIRKZEE



**MANCHESTER,** ENGLAND

MANCHESTER United inaweza kubakia peke yake katika kinyang'anyiro cha kumsajili Joshua Zirkzee kwani AC Milan sasa inaangalia washambuliaji wengine badala yake, huku Romelu Lukaku akipewa chaguo la kwanza, ripoti imedai.

90min ilifichua kwa mara ya kwanza Januari kwamba Zirkzee alikuwa kwenye rada za United kabla ya dirisha la usajili la majira ya joto.

Ripoti kutoka England zilidai kwamba 'Mashetani Wekundu' hao walikuwa wakiendeleza nia yao ya kumnunua mshambuliaji huyo wa Bologna.

Mkataba wake una kipengele cha kuruhusiwa kuondoka kwa kiasi cha pauni milioni 34, lakini masharti ya hakika na ada za wakala zimezuia makubaliano kamili kufikiwa hadi sasa, huku ikidaiwa kuwa huenda isiwe tatizo kwa United.

Gazzetta dello Sport liliandika kwamba Milan hatimaye haiko tayari kulipa ada ya wakala ya pauni milioni 12.7 zinazohitajika ili kukamilisha mpango huo, na kwa hiyo wanachunguza chaguzi zingine.

Jina moja linalozingatiwa San Siro ni Lukaku, ambaye anatarajiwa kuondoka Chelsea baada ya kukaa kwa mkopo wa miaka miwili katika Klabu ya Inter Milan na AS Roma.

Hata hivyo, dili la Lukaku kuwa gumu kutokana na nia ya Napoli, huku Antonio Conte akitarajia kuungana tena na mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ubelgiji.

Washambuliaji wengine ambao Milan inawaangalia ni pamoja na Samu Omorodion wa Atletico Madrid na Jonathan David wa Lille.

## Sesko aguswa kuhusishwa EPL

**MUNICH,** UJERUMANI

BENJAMIN Sesko amesema anafuraha kuvutiwa na vigogo kadhaa wa Ligi Kuu England baada ya kusaini mkataba mpya na RB Leipzig.

Licha ya kuwindwa na Arsenal, Chelsea na Manchester United msimu huu wa majira ya joto, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, alichagua kuongeza muda wake wa kukaa na 'Die Roten Bullen' hao ili kujiendeleza zaidi chini ya Kocha Marco Rose.

Sesko ametikisa nyavu mara 18 katika mechi 42 akiwa na Leipzig hadi sasa na ana mabao mengine 11 katika mechi 31 alizoicheza Slovenia.

Akitafakari juu ya uvumi kuhusu mustakabali wake, Sesko aliwaambia waandishi wa habari: „Kusema ukweli, pamoja na shinikizo, niliweka upande mzuri.

"Ni aina nzuri ya shinikizo. Ukipata fursa ambayo watu wanaweza kukuzungumzia, haijalishi ni nzuri au mbaya, kuna kitu kuhusu wewe na ina maana nimefanya kitu kizuri huko nyuma na watu wanazungumza juu yako.

"Siku zote ninaiweka kwa upande mzuri na ninafurahi kuwa sehemu ya hii."

Sesko bado hajafunga bao kwenye Euro 2024, lakini taifa lake limefanya vema, na kupata sare dhidi ya Denmark na Serbia.

## Italia sasa inahitaji maboresho - Kocha

**BERLIN,** ITALIA

KOCHA wa Italia, Luciano Spalletti, alisifu tabia ya kuomba ya wachezaji wake katika kuokoa pointi kwa bao la kusawazisha dakika ya 98 dhidi ya Croatia Jumatatu na kujikatia tiketi ya hatua 16-bora ya michuano ya Ulaya, lakini akasema kuna nafasi kubwa ya kuboresha kikosi.

Mchezaji aliyetokea benchi, Mattia Zaccagni, alifunga bao na kupata sare ya 1-1 katika Kundi B huku mabingwa watetezi Italia watachuana na Uswisi mjini Berlin Jumamosi, lakini Spalletti alionekana kukerwa na maswali kadhaa katika mkutano na waandishi wa habari baada ya mechi hiyo.

"Tulistahili kupitia usiku wa leo (juzi) kulingana na kile tulichozalisha huko nje. Tulikuwa laini kidogo wakati wa mchezo, hatukucheza soka letu bora," alisema kocha huyo wa zamani wa Napoli.

"Lakini ilikuwa ngumu kupita katika kundi hili. Hispania ni wazuri, Croatia ni bora. Unaposhuka chini ya viwango vya chini kama tulivyofanya katika kipindi cha kwanza, ni kwa sababu tunahisi shinikizo la jinsi mchezo ulivyo muhimu.




"Kwa sababu vinginevyo haiwezekani. Lakini kufikia sasa kila kitu wachezaji wamefanya kwenye Euro kimekuwa kikiimarika.

Alipendekeza wachezaji wake wanatakiwa kuimarika kimwili kabla ya raundi ya mtoano.

„Kila kunapokuwa na changamoto au 50-50, hatushindi hata kidogo, sio swali la kiufundi, inakuja kwa uzoefu, kuingia kwenye changamoto hizi za mwili na kuwa tayari kufanya kazi. Tunahitaji kujiboresha.

Spalletti, alifurahishwa na timu yake kuweza kudumisha umbo lao walipomaliza mchezo na wachezaji sita washambuliaji katika kusaka bao la kusawazisha.

"Wachezaji waliotokea benchi walikuwa wakubwa, waliocheza dakika 10 za mwisho walikuwa muhimu. Waliweka sura hiyo licha ya kwamba tulikuwa washambuliaji wakubwa. Tulijua hatuwezi kuruhusu bao la pili au la tatu, lakini pia kulikuwa na kushambulia."

# AZAM KUJICHIMBIA MOROCCO KUJIANDAA LIGI YA MABINGWA

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

KLABU ya Azam FC, imetangaza rasmi kuwa kambi yake ya kujiandaa na msimu ujao wa mashindano itakuwa nchini Morocco.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano, Thabit Zacharia maarufu Zaka Zakazi, jana alisema maandalizi yao ya msimu mpya (pre season) watafanyia nchini humo kwa ajili ya kujiandaa na Ligi Kuu Tanzania Bara, Kombe la FA na safari hii Ligi ya Mabingwa Afrika ambayo wataicheza kwa mara ya kwanza baada ya misimu 10.

Mara ya mwisho kwa Azam kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika ilikuwa ni msimu wa 2013/14 ilipotwaa Ubingwa wa Tanzania Bara.

Zaka Zakazi alisema wachezaji wa timu hiyo wa zamani na wapya wataanza kuripoti kuanzia Julai Mosi, na tarehe tano wataanza mazoezi kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

"Tutafanya mazoezi Chamazi, hadi tarehe saba tutakwenda Zanzibar, tukifika tutafanya mazoezi siku hiyo hiyo hadi Julai 13, tutarudi Dar na tarehe 14 tutaondoka nchini Morocco kuweka kambi ndefu sasa na hiyo ndiyo ‚pre season' yetu kwa msimu huu," alisema.

Alisema watakaa nchini Morocco hadi mwishoni mwa mwezi Julai ndipo watakaporejea, tayari kwa kufungua msimu mpya wa mashindano.

"Tutakuwa kule mpaka mwishoni mwa Julai tutarejea nchini kuja kumalizia maandalizi ya mwisho kabla ya kufungua msimu rasmi kwa mechi za Ngao ya Jamii, nadhani hapo kila kitu kitakuwa kiko tayari kwa Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Afrika ambayo tunaipa kipaumbele kwani ni muda mrefu hatujashiriki," alisema Zaka.

Azam imetangaza kufanya ‚pre season' yake, siku chache baada ya Klabu za Simba na Yanga kutangaza zitakapokwenda kuweka kambi.

Simba imatangaza rasmi kuwa mwanzoni mwa Julai inatarajia kwenda kwenye Jiji la Ismailia nchini Misri kwa ajili ya kuweka kambi ya mwanzo wa msimu, huku Yanga ikisema safari hii itakwenda ‚pre seasons' Ulaya, huku pia ikiwa na ziara nchini Kenya na Afrika Kusini ambako inatarajia kucheza mechi za kirafiki dhidi ya Mamelodi Sundowns na Kaizer Chiefs.

# Maandalizi mashindano ya Gofu Lina Nkya Tour yashika kasi

**Na Mwandishi Wetu**

WACHEZAJI wa gofu wa kulipwa, Nuru Mollel aliyeshinda raundi ya kwanza katika viwanja vya TPC Moshi na Hassan Kadio aliyeutwaa ubingwa wa raundi ya pili mjini Morogoro, ndiyo vinara katika orodha ya wachezaji waliosajiliwa kucheza katika raundi ya tatu ya mashindano ya kumuenzi mchezaji wa gofu kwa wanawake, Lina Nkya, mjini Arusha katikati ya mwezi ujao.

Mashindano hayo ya aina yake yanayoandaliwa kwa pamoja na familia ya Nkya kwa kushirikiana na Chama cha Gofu cha Wanawake Tanzania (TLGU) na kile cha wachezaji wa Kulipwa (TPGA), yanakutanisha wakali wa gofu ya kulipwa na ridhaa nchini.

Arusha Gymkhana wanakuwa wenyeji wa raundi ya tatu baada ya zile mbili za mafanikio makubwa katika viwanja vya TPC na Morogoro.

Akizungumza na mwandishi wetu jana, Mkurugenzi wa Mashindano hayo, Yasmin Chali, ametaka wale ambao hawajajiandikisha kufanya hivyo mapema maana nafasi zilizosalia ni chache.

Alisema mashindano yataanza rasmi Julai 11 na kumalizika Julai 14, mwaka huu, mjini Arusha.

Chali alisema jumla ya mashimo 72 yatachezwa katika siku hizo nne, ikiwa na maana kutakuwa na mbio za mashimo 18 kila siku.

"Kila kitu kinakwenda vema katika maandalizi yetu na viwanja vya Gofu vya Arusha viko katika ubora unaotakiwa kwa ajili ya mashindano haya," alisisitiza Chali.

Aliongeza kuwa pia kutakuwa na mashindano kwa ajili ya wachezaji wa kawaida na kitengo hiki kwa mujibu wa Chali kinajulikana kama ‚Subsidiary Event'.




Mmoja wa washiriki wa mashindano ya Gofu Lina Tour, Madina Idd, akiwa mazoezi. Mashindano hayo yatafanyika viwanja vya Gymkhana Arusha kuanzia Julai 11, mwaka huu. **MPIGAPICHA WETU**

## Yanga kushusha beki la Enyimba

INATOKA UK. 24

boresho ya kikosi chetu cha msimu wa 2024/25, pia kuwatangazia wanachama na mashabiki wa Yanga ratiba nzima ya ‚pre season' yetu, sasa hivi tuacheni tu tule bata kwa sababu ya kazi kubwa ambayo tumeifanya msimu uliomalizika.

"Wanachama na mashabiki wa Yanga wala wasiwe na wasiwasi, ikifika siku hiyo tutaanza kutangaza idadi ya wachezaji ambao watasalia kwenye kikosi, kutoa taarifa ya wachezaji ambao wanaondoka, lakini kuwajulisha majembe mapya ambayo yameingia ndani ya kikosi chetu," alisema Kamwe.

## Simba, straika wa Asante Kotoko safi

INATOKA UK. 24

alikataa," alisema mtoa taarifa wetu.
Habari zinasema ushawishi wa wachezaji hao ndiyo kwa kiasi kikubwa umemfanya kuichagua Simba badala ya FC Petrocub ya nchini Moldovia ambayo mara kwa mara huwa inashiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua za awali.
Licha ya timu yake kumaliza nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi ya Ghana, Mukwala amemaliza akiwa nafasi ya pili kwenye orodha ya wafungaji bora nchini humo, akipachika mabao 14, akiongozwa na mshindi wa kiatu cha dhahabu msimu uliomalizika, Stephen Amankona wa Berekum Chelsea FC alimaliza na mabao 19.
Straika huyo anatajwa kwenda kuchukua nafasi ya Pa Omari Jobe ambaye taarifa zinaeleza kuwa atatolewa kwa mkopo baada ya kushindwa kuonyesha makali yake tangu aliposajiliwa katikati ya msimu uliomalizika.
Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, amewataka wanachama na mashabiki wa Simba kuwa watulivu kwani kila mchezaji aliyesajiliwa atatangazwa kwa nyakati tofauti, akitamba kuwa safari hii wanafanya usajili mkubwa.
"Muda utaongea, tumeshaanza kutoa ‚thank you', kutangaza wachezaji wapya tuliowasajili, na tunaowaongeza mikataba, kwa hiyo yeyote ambaye tumemsajili tutamtangaza wenyewe, mashabiki wavute subira, safari hii Mo mwenyewe ndiye anaongoza kikosi cha usajili, hii inadhihirisha kuwa meshine zitakazoshuka zitakuwa ni mashine kweli kweli," alisema.
Wakati huo huo, klabu hiyo imetangaza rasmi kumwongeza mkataba wa miaka miwili mingine kiungo wake, Mzamiru Yassin.
Kiungo huyo amekuwa na timu hiyo kwa miaka minane sasa, tangu alipojiunga nayo mwaka 2016 akitokea Mtibwa Sugar.

Michezo
Nipashe
Jumatano Juni 26, 2024

## Modric: Bado nataka kuendelea kucheza



UKURASA 21



Beki wa kati wa Albania, Arlind Ajeti, akiucheza mpira kwa kichwa dhidi ya beki wa Hispania, Daniel Vivian, wakati wa mechi ya Kundi B ya michuano ya Euro, iliyopigwa Ujerumani juzi na Wahispania kushinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA KUSHUSHA BEKI LA ENYIMBA

## Ni baada ya Gamondi kutaka beki mrefu, Job kubadilishiwa majukumu huku Mwamnyeto...

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA kukiimarisha kikosi chake kwa ajili ya msimu ujao wa mashindano, Yanga imepiga hodi Klabu ya Enyimba kutaka kumsajili beki wa kati wa timu hiyo, Chikamso Okechukwu, mwenye umri wa miaka 22.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema kuwa tayari viongozi wa Yanga wameanzisha mazungumzo na wenzao wa Enyimba kuona uwezekano wa kuipata saini ya mchezaji huyo kwani bado ana mkataba na kikosi hicho cha Mabingwa wa Afrika 2003.

Beki huyo raia wa Nigeria anatajwa kuja kuchukua nafasi ya Gift Fredy raia wa Uganda ambaye ameshindwa kumshawishi Kocha Miguel Gamondi tangu alipojiunga kutoka SC Villa ambapo amekuwa hana namba ya kudumu ndani ya kikosi hicho.

"Hapa kuna mawili, anasajiliwa kuchukua nafasi iliyoachwa wazi na Gift, pia hakuna uhakika sana kama Mwamnyeto (Bakari), atabaki japo mazungumzo yanaendelea, lakini hata kama akibaki, Okechukwu anatakiwa kwa udi na uvumba, labda dili liharibike mwishoni.

Kocha anataka mara nyingi Dickson Job acheze pembeni na siyo kati kwa sababu ya hatari ya mipira ya juu, kati pale acheze lakini isiwe ndiyo namba yake ya kudumu, anamtaka beki mrefu aje kutengeneza pacha na Bacca (Ibrahim Hamad).

Okechukwu ndiye beki tegemeo kwa sasa kwenye kikosi cha Enyimba ambacho kilimaliza ligi kikiwa nafasi ya tatu Ligi Kuu ya Nigeria msimu uliomalizika.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, amesema kwa sasa hawawezi kuweka wazi wachezaji ambao imewasajili au kuwaacha mpaka itakapofika Julai Mosi kama alivyoahidi huko nyuma.

"Ikifika Julai Mosi, sisi Yanga ndiyo tutarudi mzigoni, sasa hivi tuko mapumzikoni, tunainjoi likizo zetu, lakini ikifika siku hiyo tunaanza kuvaa sura ya kazi. Tutaanza ma-

INAENDELEA UK. 23

## Simba, straika wa Asante Kotoko safi

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imetajwa kumalizana na straika Steven Mukwala anayekipiga na Klabu ya Asante Kotoko ya Ghana kwa ajili ya kutibu tatizo sugu la kupachika mabao.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema kuwa mchezaji huyo amepatikana kutokana na maskauti walioteuliwa na Mwekezaji, rais wa Heshima na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Mohamed ,Mo' Dewji, ambaye safari hii ameingia kazini mwenyewe kuhakikisha wachezaji bora wanapatikana.

Chanzo hicho kimebainisha kuwa straika huyo anaweza kutibu tatizo la ushambuliaji ndani ya klabu hiyo, kwani pamoja na kuwa tegemeo kwenye klabu hiyo, lakini anaichezea Timu ya Taifa ya Uganda, The Cranes.

"Nadhani ni chaguo sahihi, ana miaka 24 sasa, huyu kijana ndiye alikwenda kumaliza utawala wa kina Emmanuel Okwi na Farouk Miya kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya Uganda, uzuri na yeye ameonekana kufurahia kuchezea Simba kutokana na rekodi nzuri ya wachezaji wa timu hiyo walioichezea miaka ya nyuma.

"Ameongea na kina Okwi na Patrick Ochan ambao walicheza Simba na kupata mafanikio makubwa ndani na nje ya uwanja kwa hiyo na yeye amevutiwa, ndiyo maana klabu yake ilitaka kumwongezea mkataba kabla ya msimu kumalizika lakini mwenyewe

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >